# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

83. Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa Mtume (na yakawatulilikia kuwa ni kweli), utaona macho yao yanamiminika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua; wanasema: "Mola wetu! Tumeamini, basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia (ukweli huu)."

وَإِذَا سَمِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَى الرَّسُولِ تَرَىٰ
أَعْيُنَهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ مِمَّا عَرَفُوا مِنَ الْحَقِّ ۖ
يَقُولُونَ رَبَّنَا آمَنَّا فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨٣﴾

84. (Na wakilaumiwa kwa kusilimu kwao husema): "Na kwa nini tusimwamini Mwenyezi Mungu na haki iliyotufikia, na hali tunatumai Mola wetu atuingize (Peponi) pamoja na watu wema?"

وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا جَاءَنَا مِنَ الْحَقِّ
وَنَطْمَعُ أَن يُدْخِلَنَا رَبُّنَا مَعَ الْقَوْمِ الصَّالِحِينَ ﴿٨٤﴾

85. Basi Mwenyezi Mungu atawalipa—kwa yale waliyoyasema—Bustani (Pepo) zipitazo mbele yake mito; humo watakaa milele. Na hayo ndiyo malipo ya wafanyao wema.

فَأَثَابَهُمُ اللَّهُ بِمَا قَالُوا جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا
الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَذَٰلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٥﴾

86. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Aya zetu, hao ndio watu wa Motoni.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ
الْجَحِيمِ ﴿٨٦﴾

87. Enyi mlioamini! Msiharimishe vizuri alivyokuhahalishieni Mwenyezi Mungu, wala msiruke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحَرِّمُوا طَيِّبَاتِ مَا
أَحَلَّ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ
الْمُعْتَدِينَ ﴿٨٧﴾

88. Na kuleni katika vile alivyokuruzukuni Mwenyezi Mungu vilivyo halali na vizuri; na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye nyinyi mnamwamini.

وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ
الَّذِي أَنتُم بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾

89. Mwenyezi Mungu hatakuteseni kwa viapo vyenu vya upuzi, lakini atakukamateni kwa viapo mlivyoapa kwa nia mlioifunga barabara. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha katikati mnachowalisha watu wa majumbani mwenu, au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa. Lakini

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِن
يُؤَاخِذُكُم بِمَا عَقَّدتُّمُ الْأَيْمَانَ ۖ فَكَفَّارَتُهُ
إِطْعَامُ عَشَرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعِمُونَ
أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ ۖ فَمَن لَّمْ يَجِدْ

---

wa Mungu; na (b) Manasara hata wakamfanya Nabii Isa (i) Mungu au (ii) Mtoto wa Mungu au (iii) Mmoja katika hao waungu wao watatu.

Na Mtume akatutahadharisha kupindukia mipaka katika kumsifu.

Na juu ya hivi tunapindukia, kama vile kusema:-

Lau kuwa si yeye wasingeumbwa Mitume wo wote,
usingeumbwa ulimwengu wala Pepo wala . . .
Na kuwa ameumbwa kwa nafsi ya nuru ya Mungu . . .
Hakuna maneno haya katika Qurani wala Hadithi Sahihi za Mtume.

78, 79. Unatajwa hapa ubaya wa (a) kutoamrisha mema na (b) kutokataza mabaya, kwani pasina kufanya hivi ubaya unazidi kutangaa. Lazima juu ya kila mjuzi aondoshe mabaya kwa (i) Mkono wake; kama hawezi basi (ii) akataze kwa ulimi wake. Hata hili akiwa anaogopa ndiyo (iii) achukie kwa moyo wake. Lakini hii ni daraja ndogo kabisa ya Uislamu—unaogopa hata kusema!

Wametia makadiyani ukafiri wao tena katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni 79 wakaandika hivi: "Yesu alipigiliwa msalabani." Tumebainisha katika Aya waliyoifanya ya 157 ya *Suratun Nisaa* ukafiri wao huu wa kumpinga Mwenyezi Mungu wakasema — kama Manasara — kuwa Nabii Isa amesulubiwa; na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anasema: "*Wamaa salabuuhu*" (Hawakumsulibu).

80-81. Unatajwa ubaya wa Mayahudi na Manasara kuwa wanakhiari kuwafanya makafiri vipenzi vyao kuliko Waislamu, na hali ya kuwa wanajua kuwa Waislamu ndio wazuri na ndio walio katika haki; lakini husuda yao

فَصِيَامُ ثَلٰثَةِ اَيَّامٍ ذٰلِكَ كَفَّارَةُ اَيْمَانِكُمْ اِذَا
حَلَفْتُمْ وَاحْفَظُوْٓا اَيْمَانَكُمْ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ
لَكُمْ اٰيٰتِهٖ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٨٩﴾

asiyeweza kupata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapoapa. Na vilindeni viapo vyenu, (msiape kisha msitimize). Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kushukuru.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ
وَالْاَنْصَابُ وَالْاَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطٰنِ
فَاجْتَنِبُوْهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٩٠﴾

90. Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishare ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa).

اِنَّمَا يُرِيْدُ الشَّيْطٰنُ اَنْ يُّوْقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ
وَالْبَغْضَآءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ
ذِكْرِ اللّٰهِ وَعَنِ الصَّلٰوةِ فَهَلْ اَنْتُمْ مُّنْتَهُوْنَ ﴿٩١﴾

91. Hakika Shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kusali. Basi je, mtaacha (mabaya hayo)?

وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ وَاحْذَرُوْا
فَاِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوْٓا اَنَّمَا عَلٰى رَسُوْلِنَا
الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿٩٢﴾

92. Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na tahadharini (na kukhalifu amri zao). Na mkikengeuka basi jueni ya kwamba juu ya Mtume wetu ni kufikisha tu ujumbe) waziwazi. (Na akishafikisha hana lawama; lawama juu yenu).

لَيْسَ عَلَى الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ جُنَاحٌ
فِيْمَا طَعِمُوْٓا اِذَا مَا اتَّقَوْا وَّاٰمَنُوْا وَعَمِلُوا
الصّٰلِحٰتِ ثُمَّ اتَّقَوْا وَّاٰمَنُوْا ثُمَّ اتَّقَوْا وَّ
اَحْسَنُوْا وَاللّٰهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٩٣﴾ ع

93. Si dhambi juu ya walioamini na wakatenda mema kwa vile walivyovila (kabla ya kuharimishwa) maadamu wakimcha (kwa vile alivyowaharimishia wakati huo) na wakiamini (alivyowaamrisha wakati huo) na wakitenda mema. Tena wakamcha (alipowakataza mengine) na kuamini (alipowaamrisha mengine). Tena wakamcha (vile vile alipowakataza makatazo mengine) na wakafanya mema (mengine aliyowaamrisha). Na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَيَبْلُوَنَّكُمُ اللّٰهُ بِشَيْءٍ مِّنَ
الصَّيْدِ تَنَالُهٗٓ اَيْدِيْكُمْ وَرِمَاحُكُمْ لِيَعْلَمَ اللّٰهُ مَنْ

94. Enyi mlioamini! Mwenyezi Mungu atakujaribuni kwa baadhi ya wanyama wa kuwinda inayowafikia mikono yenu na mikuki yenu, ili Mwenyezi Mungu ajulishe ni nani anayemwogopa

---

kubwa juu ya Waislamu; basi hata wakiwa vipi, wanawachukia tu.

Na makafiri wengine ndio vivi hivi. Wanawachukia Waislamu zaidi kuliko wanavyowachukia wenye dini nyingine.

82. Hapa inaonyeshwa kuwa walio haijambo kidogo katika kuwachukia Waislamu ni Manasara. Na zimetajwa kidogo hapa sifa zao, na katika baadhi ya Aya zifuwatazo.

83. Hapa wanasifiwa Wakristo kama walivyotukanwa Mayahudi nyuma katika Aya ya 82 na nyinginezo. Manasara wengi wamesilimu — na mpaka sasa wanaendelea kusilimu katika pande zote za ulimwengu. Lakini Mayahudi wachache kabisa waliosilimu.

87. Waarabu katika ukafiri wao walijiharimishia kula baadhi ya vyakula na baadhi ya nyama, kama (a) Jike aliyezaa mimba kumi. Basi wakisema haramu kuliwa nyama yake, haifai kuchinjwa; (b) Dume lililopanda likazalisha majike wengi; (c) Dume aliyezaliwa pamoja na jike; (d) Mnyama yo yote aliyewekwa nadhiri kuwa huyo haramu kumchinja.

Basi baadhi ya Waislamu juu ya kusilimu kwao walikuwa wakiona taabu kula wale wanyama ambao katika

(Mwenyezi Mungu) japo hamwoni. Basi atakayeruka mipaka (akawawinda) baada ya hayo mlioambiwa, atapata adhabu inayoumiza.

يَخَافُهُ بِالْغَيْبِ ۚ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَلَهُ
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٩٤﴾

95. Enyi mlioamini! Msiue mawindo na hali (ya kuwa) mumo katika Hija au Umra. Na miongoni mwenu atakayemwua kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa kwa (kuchinja) kilicho sawa na alichokiua, katika wanyama wanaofugwa, kama watakavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu mnyama huyo apelekwe iliko Kaaba (akachinjwe huko na kutasadakiwa masikini); au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake (hili). Mwenyezi Mungu amekwishayafuta yaliyopita; lakini atakayefanya tena Mwenyezi Mungu atampa adhabu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu (na) Mwenye kuadhibu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنْتُمْ حُرُمٌ ۚ
وَمَنْ قَتَلَهُ مِنْكُمْ مُتَعَمِّدًا فَجَزَاءٌ مِثْلُ مَا قَتَلَ
مِنَ النَّعَمِ يَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِنْكُمْ هَدْيًا بَالِغَ
الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّارَةٌ طَعَامُ مَسَاكِينَ أَوْ عَدْلُ ذَٰلِكَ
صِيَامًا لِيَذُوقَ وَبَالَ أَمْرِهِ ۗ عَفَا اللَّهُ عَمَّا
سَلَفَ ۚ وَمَنْ عَادَ فَيَنْتَقِمُ اللَّهُ مِنْهُ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
ذُو انْتِقَامٍ ﴿٩٥﴾

96. Nyinyi mumehalalishiwa mawindo ya bahari na chakula chake (yaani kilichokutikana kimekufa bila ya kuvuliwa), ndiyo posho yenu (nyinyi msiokuwa safarini) na kwa wasafiri. Na mumeharimishiwa mawindo ya bara maadamu

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَاعًا لَكُمْ
وَلِلسَّيَّارَةِ ۖ وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ

---

ukafiri wao wakiitakidi kuwa haramu kuliwa. Ndiyo wanakatazwa hapa kujiharimishia alichowahalalishia Mwenyezi Mungu.

89. Inataka mtu anaposema neno lake alitimize maadamu ni neno la kheri, khasa anapoliakidisha kwa kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu. Kama kusema kwa dhati yake kweli kweli "Wallahi! Nitafanya jambo fulani" (Nalo ni zuri). Basi kama hajalifanya itampasa ima (a) Ampe uungwana mmoja katika watumwa wake, kama anao watumwa au (b) Awape chakula masikini kumi — kila mmoja kibaba (au kisaga) cha chakula wanachokila wenyewe; sio chakula duni au (c) Awape nguo masikini kumi — kama kumpa kila mtu kikoi au kanzu au fulana. Na aliye masikini asiyeweza haya afunge siku 3.

Na vile vile akiapa kwa dhati yake akasema "Wallahi Sifanyi jambo fulani" (ambalo ni baya) basi akifanya yatampasa haya.

*N.B.* — Kibaba Ratili na robo.

90. Habari ya Ulevi imetajwa katika Aya ya 219 ya *Suratil Baqarah* na imetajwa katika Aya ya 43 ya *Suratin Nisaa*.

93. Aya hizi za kukataza Ulevi kwa tashdidi hii zimeteremka mwaka wa sita wa Al Hijra baada ya kuwa Masahaba wengi wamekufa na hali ya kuwa wakilewa. Basi Masahaba wenziwao wakawakhofia sana nini itakuwa hali yao Kiyama. Ndio wakajibiwa hapa kuwa hapana lawama juu yao kwani ilikuwa haujaharimishwa siku hizo. Wao ilikuwa juu yao kujiepusha na hayo yaliyokuwa wamekatazwa siku hizo. Nao walikuwa wakijiepusha na kila lililokuwa likikatazwa, na wakifanya kila lililokuwa likiamrishwa. Basi yale ndiyo yaliyokuwa wajibu juu yao, siyo haya ya kuacha ulevi.

Aya hii waliyoifanya ni ya 94 inafahamisha ile Naskhi aliyoikubalisha Mwenyezi Mungu akaitaja katika Qurani — kuleta amri kidogo kidogo na makatazo kidogo kidogo; na wakaikataa. Na sisi tukawavunja katika maelezo ya Aya ya 106 ya *Suratul Baqarah*. Basi hapa wanageuzageuza tafsiri ya Aya hii ifahamishe uwongo wao huo. Lakini wapi!

94. Mwenyezi Mungu huwafanyia mtihani waja Wake kwa lo lote lile atakalo aonyeshe walikuwa waja hawa wametii, wamefuata waliyoambiwa, au hawakutii.

Nyuma huko alilifanyia mtihani jeshi alilokuwamo Nabii Daudi kuwa litashikwa na kiu kali kabisa, na litakutana na mto wa maji mengi mazuri lakini halina ruhusa kunywa na kukata kiu katika mto huo. Ruhusa aliyopewa kila

nyinyi mumo katika kuhiji, au umra. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mtakusanywa kwake.

حُرُمًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٩٦﴾

97. Mwenyezi Mungu ameifanya Kaaba—hii Nyumba tukufu—kuwa tengenezo la (maisha ya) watu na (akaifanya) ile miezi mine mitukufu (pia tengenezo la maisha ya watu) na kule kupeleka wanyama Makka, na kujitia vigwe (vya kuonyesha kuwa wao Mahujaji; yote hayo ni kwa ajili ya tengenezo la maisha ya watu. Amefanya) haya kwa sababu mjue ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo katika ardhi, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

جَعَلَ اللَّهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ قِيَامًا لِلنَّاسِ وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَالْهَدْيَ وَالْقَلَائِدَ ۚ ذَٰلِكَ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٩٧﴾

98. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu (pia kwa wanaotubia).

اعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ وَأَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٨﴾

99. Hakuna juu ya Mtume ila kufikisha tu, na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha.

مَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٩٩﴾

100. Sema (Umwambie kila mtu): "Hawawi sawa wabaya na wema, hata huo wingi wa wabaya ukikufurahisha (usimili katika wingi huo). Basi mcheni Mwenyezi Mungu enyi wenye akili (msende katika ubaya japo ndiko kwenye wingi) ili mpate kufuzu.

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ ۚ فَاتَّقُوا اللَّهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٠٠﴾ ع

101. Enyi mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na kama mtayauliza, maadamu inateremshwa Qurani mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu amesamehe hayo. Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mpole sana.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِنْ تُبْدَ لَكُمْ تَسُؤْكُمْ وَإِنْ تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنَزَّلُ الْقُرْآنُ تُبْدَ لَكُمْ عَفَا اللَّهُ عَنْهَا ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٠١﴾

---

mmoja katika hao ni kuteka maji funda tu katika mkono wake anywe lile lile tu basi, likimkata kiu lisimkate. Basi wengi katika hao walikhalifu amri hiyo wakayapapia kweli kweli.

Kisa hiki kimetajwa katika Aya ya 249 ya *Suratil Baqarah.*

Basi na Nabii Muhammad (s.a.w.) katika mwaka wa sabaa wa Al Hijra alipotoka na jeshi lake la watu elfu wa khamsumia wanakwenda kufanya umra, Mwenyezi Mungu aliwaharimishia kuwinda kinyama cho chote cha barani. Na akawaambia kuwa atawafanyia mtihani wa kuwawekea chekwa wanyama hao katika kila njia watakayoyopita. Watakuwa chekwa kila upande na wengi kabisa wa kuweza kwa urahisi kupigwa kwa mikuki; bali na kukamatwa kwa mikono pia. Lakini wakaambiwa hawana ruhusa kuwagusa.

Basi walifanyiwa haya wakayakuta hayo waliyoambiwa; lakini wote walivuka salama; hakuna aliyekhalifu hata mmoja.

95. Baada ya kuvuka mtihani ule uliotajwa katika Aya ya 94 imeambiwa kuwa sasa mtu akiua kiwinda naye yuko katika Hija au umra basi:-

(1) Atachinja kinyama cha kufuga kinachoshabihiana kwa sura na hicho kiwinda alichokiua.

(a) Akiua mbuni atachinja ngamia atoe nyama yake kuwa sadaka kwa masikini;
(b) Akiua nyati au punda milia atachinja ng'ombe atoe nyama yake sadaka;
(c) Akiua paa atachinja mbuzi atoe sadaka nyama yake.

Au

(2) Kitatiwa thamani hicho kinyama kinachoshabihi kiwinda hicho. Aambiwe kununua, kwa thamani hiyo yote, chakula cha chembechembe (nafaka) kinacholiwa sana katika nchi hiyo. Ampe kila masikini kibaba kimoja.

102. Watu wa kabla yenu waliyauliza, kisha wakawa wenye kuyakataa.

103. Mwenyezi Mungu hakujaalia (uharamu wo wote) juu ya Bahira wala Saiba wala Wasila wala Hami; lakini waliokufuru wanamtungia uwongo Mwenyezi Mungu, na wengi katika wao hawatumii akili (hata kidogo).

104. Na wanapoambiwa, "Njo-oni katika hukumu alizoziteremsha Mwenyezi Mungu na (anazozisema) Mtume," husema: "Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo baba zetu." Je, hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka (watawafuata tu)?

105. Enyi mlioamini! Lililo lazima juu yenu ni nafsi zenu. Hawakudhuruni waliopotoka ikiwa mumeongoka. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; basi atakwambieni yale mliyokuwa mkiyatenda.

106. Enyi mlioamini! Wekeni mawasii wawili wenye uadilifu miongoni mwenu (Waislamu wenzenu), wakati wa kuusia, yanapomfikia mauti mmoja wenu. Au (wekeni mashahidi) wengine wawili wasiokuwa katika nyinyi (wasiokuwa Waislamu) mnapokuwa safarini (na hapana waislamu mbele yenu), na msiba wa mauti ukakufikieni. (Nyinyi mahakimu) Mtawasimamisha wawili hao baada ya Sala, na waape kwa Mwenyezi Mungu kama mkiwa na shaka (katika wasia huo walioutaja hao mashahidi), (Waseme katika kuapa kwao): "Hatukupokea cho chote (ikiwa tumebadilisha haya) ingawa ni jamaa (yetu) wala hatutaficha ushuhuda wa Mwenyezi Mungu; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi (kubwa)."

قَدْ سَأَلَهَا قَوْمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ثُمَّ أَصْبَحُوا بِهَا
كَافِرِينَ ﴿١٠٢﴾
مَا جَعَلَ اللَّهُ مِن بَحِيرَةٍ وَلَا سَائِبَةٍ
وَلَا وَصِيلَةٍ وَلَا حَامٍ ۙ وَلَٰكِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا
يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۖ وَأَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٣﴾
وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّهُ وَإِلَى
الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ۚ
أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٠٤﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ ۖ لَا يَضُرُّكُم
مَّن ضَلَّ إِذَا اهْتَدَيْتُمْ ۚ إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا
فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا شَهَادَةُ بَيْنِكُمْ إِذَا حَضَرَ
أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ حِينَ الْوَصِيَّةِ اثْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ
مِّنكُمْ أَوْ آخَرَانِ مِنْ غَيْرِكُمْ إِنْ أَنتُمْ ضَرَبْتُمْ فِي
الْأَرْضِ فَأَصَابَتْكُم مُّصِيبَةُ الْمَوْتِ ۚ تَحْبِسُونَهُمَا
مِن بَعْدِ الصَّلَاةِ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّهِ إِنِ ارْتَبْتُمْ لَا
نَشْتَرِي بِهِ ثَمَنًا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۙ وَلَا نَكْتُمُ شَهَادَةَ
اللَّهِ إِنَّا إِذًا لَّمِنَ الْآثِمِينَ ﴿١٠٦﴾

Au

(3) Afunge kwa idadi ya vibaba hivyo. Kama ikikadiriwa kwa bei ya mbuzi mmoja vinaweza kunulika vibaba 40 vya mchele basi atafunga siku 40; na kama hivi.

96. Mahujaji wanaharimishiwa viwindwa vya barani. Ama vya baharini hawaharimishiwi.

*N.B.* — Na viwindwa vya baharini ni halali kwa kila mtu — vikivuliwa na vikikutikana vinaolea vimekwisha kufa. Pia halali kuvila maadamu havitakudhuru. Na takriba vinyama vya majini (maji matamu na ya chumvi) vyote ni halali kuvila ila Chura.

97. Maisha Bara Arabu yalikuwa si ya kuishika — ilikuwa kunyang'anyana na kupigana na kuuana tu dom daima ila: (a) Wakihishimu Al Kaaba na Ardhi iliyo karibu na Al Kaaba (Makka na pambizo zake). Hapo hapakuwa pakinyang'anywa mtu wala kupigwa wala kuuawa. Na (b) Wakihishimu vinyama vinavyochungwa kupelekwa Makka kwenda kutolewa sadaka. Basi wakiwahishimu na wale wanaowachunga. Basi hawakuwa wakitaabishwa kwa lo lote. Na (c) vile vile waliojitia alama za kuwa wao wanakwenda kuhiji. Na (d) Wakihishimu miezi mine — Mfunguo pili, Mfunguo tatu, Mfunguo nne na Mfunguo kumi (Rajabu). Katika miezi hii walikuwa hawanyang'anyani wala hawapigani wala . . .

Ndio maana Mwenyezi Mungu akasema kuwa haya ni tengenezo la maisha ya watu — hao Waarabu.

101. Hapa Waislamu wamekatazwa kuuliza suala zisizokuwa na haja ambazo hazina faida katika dini wala dunia; wasije wakapata jawabu za kuwaudhi. Kama vile kuuliza 'Mimi mwana wa halali au mwana wa haramu?'

107. Ikigundulikana ya kwamba wawili hao wamefanya dhambi (ya kusema uwongo katika hayo waliyoyashuhudia), basi wawili wengine katika wale warithi uliowadhuru wasia huo watasimama mahali pao, waape kwa Mwenyezi Mungu (na kunena): "Ushahidi wetu ni kweli zaidi kuliko ushahidi wao, na sisi hatukufanya dhuluma; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa madhalimu.

108. Hivi inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo (vingine) baada ya viapo vyao. Na mcheni Mwenyezi Mungu na msikie (mnayoambiwa), na hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi.

109. (Kumbukeni) Siku ambayo Mwenyezi Mungu atawakusanya Mitume awaambie: "Mlijibiwa nini?" (Mitume) watasema: "Hatuijui ilimu (kama yako juu ya jambo hili wala jenginelo). Bila shaka Wewe ndiye ujuaye mambo ya siri."

110. (Kumbukeni tena) Mwenyezi Mungu atakaposema: "Ewe Isa mwana wa Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako, nilipokusaidia kwa (kukupa kuwa na wewe) roho takatifu (Jibrili), ukazungumza na watu (maneno ya nafuu) katika utoto (wako) na katika utuuzima (wako). Na (kumbuka) nilivyokufundisha kuandika na (nikakupa) Hikima na Taurati na Injili. Na kumbuka ulipotengenza kwa udongo sura za ndege kwa idhini yangu, kisha ukapuliza zikawa ndege kwa idhini yangu, na ulipowaponesha vipofu na wenye mbalanga kwa idhini yangu, na ulipowatoa (baadhi ya) wafu (makaburini mwao) kwa idhini yangu, na nilipokuzuilia wana wa Israili (wasikudhuru) ulipowafikia kwa hoja zilizo wazi; wale waliokufuru miongoni mwao wakasema. "Haya si cho chote ila ni uchawi dhahiri."

فَإِنْ عُثِرَ عَلَىٰٓ أَنَّهُمَا ٱسْتَحَقَّآ إِثْمًا فَـَٔاخَرَانِ يَقُومَانِ
مَقَامَهُمَا مِنَ ٱلَّذِينَ ٱسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ ٱلْأَوْلَيَٰنِ
فَيُقْسِمَانِ بِٱللَّهِ لَشَهَٰدَتُنَآ أَحَقُّ مِن شَهَٰدَتِهِمَا وَمَا
ٱعْتَدَيْنَآ إِنَّآ إِذًا لَّمِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ١٠٧

ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يَأْتُوا۟ بِٱلشَّهَٰدَةِ عَلَىٰ وَجْهِهَآ أَوْ يَخَافُوٓا۟
أَن تُرَدَّ أَيْمَٰنٌۢ بَعْدَ أَيْمَٰنِهِمْ ۗ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ
وَٱسْمَعُوا۟ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلْفَٰسِقِينَ ١٠٨

يَوْمَ يَجْمَعُ ٱللَّهُ ٱلرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَآ أُجِبْتُمْ ۖ قَالُوا۟
لَا عِلْمَ لَنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّٰمُ ٱلْغُيُوبِ ١٠٩

إِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ ٱذْكُرْ نِعْمَتِى
عَلَيْكَ وَعَلَىٰ وَٰلِدَتِكَ إِذْ أَيَّدتُّكَ بِرُوحِ
ٱلْقُدُسِ تُكَلِّمُ ٱلنَّاسَ فِى ٱلْمَهْدِ وَكَهْلًا ۖ وَإِذْ
عَلَّمْتُكَ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَٱلتَّوْرَىٰةَ وَٱلْإِنجِيلَ ۖ وَإِذْ
تَخْلُقُ مِنَ ٱلطِّينِ كَهَيْـَٔةِ ٱلطَّيْرِ بِإِذْنِى فَتَنفُخُ فِيهَا
فَتَكُونُ طَيْرًۢا بِإِذْنِى ۖ وَتُبْرِئُ ٱلْأَكْمَهَ وَٱلْأَبْرَصَ
بِإِذْنِى ۖ وَإِذْ تُخْرِجُ ٱلْمَوْتَىٰ بِإِذْنِى ۖ وَإِذْ كَفَفْتُ بَنِىٓ
إِسْرَٰٓءِيلَ عَنكَ إِذْ جِئْتَهُم بِٱلْبَيِّنَٰتِ فَقَالَ ٱلَّذِينَ
كَفَرُوا۟ مِنْهُمْ إِنْ هَٰذَآ إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ١١٠

Au 'Mimi nitaingia Motoni au nitaingia Peponi?' Na kama walipofaridhiwa kuhiji wakasema 'Mara ngapi ahiji mtu katika maisha yake?' Wanatakia nini kuuliza? Lililokuwa la kila mwaka mara moja — kama kufunga na kutoa zaka — walibainishiwa kuwa kila mwaka mara moja. Na lililokuwa la kila siku — kama kusali — walibainishiwa kuwa ni la kila siku. Na hii Hija haikubainishiwa kitu; basi muradi kuwa mara moja inatosha. Ya nini kutafuta tashdidi? Basi suala namna hizi Mwenyezi Mungu hazipendi.

103. Waarabu walikuwa wakiharimisha kuwala na kuwatumia wanyama hawa; na wakisema kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha hayo. Wanyama wenyewe ni hawa: (1) *Hami* — beberu lililopanda sana; (2) *Bahira* — Ngamia aliyezaa mimba kumi; (3) *Saiba* — Kondoo (au mbuzi) aliyezaa mimba tano; (4) *Wasila* — Dume aliyezaliwa pacha na jike. Na kama hawa.

105. Haya huambiwa mtu inapokuwa ametekeleza fardhi yake ya kuamrisha mema na kukataza mabaya na ikawa hasikilizwi. Basi yeye hana lawama juu ya mabaya yatakayofanywa na hao. Lawama yake ni juu ya amali zake mwenyewe sasa.

106. Uislamu unahimiza kila jambo muhimu kuliandika; kama kukopa, kuweka wakfu, kuusia na kama haya. Na ikiwa bahati mbaya mauti yamemkumba kwa ghafla anapata ruhusa ya kuwausia watu wawili wafikishe hayo ambayo ilikuwa ayaandike.

111. Na nilipowafunulia wanafunzi (wako) kwamba: "Niamini Mimi na Mtume wangu (huyu Isa)," wakasema: "Tumeamini na uwe shahidi kuwa sisi ni wanyenyekevu."

112. (Kumbuka) Wanafunzi (wako) waliposema: "Ewe Isa mwana wa Maryamu! Je, Mola wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni?" Akasema (Nabii Isa): "Mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini kweli. (Musitake miujiza)."

113. Wakasema: "Tunataka kula katika hicho na ili nyoyo zetu zitulie na tujue ya kwamba umetwambia kweli na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia (miujiza ya Mwenyezi Mungu anayowafanyia Mitume yake)."

114. Akasema Isa bin Maryamu: "Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu (Nao ni sisi) na wa mwisho wetu (Nao ni wafuasi wetu watakaokuja baada yetu wakasikia haya), na kiwe Ishara itokayo kwako, basi turuzuku, kwani wewe ndiye mbora wa wanaoruzuku."

115. Mwenyezi Mungu akasema: "Bila shaka Mimi nitakiteremsha juu yenu, lakini miongoni mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi nitamuadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yo yote katika walimwengu."

116. Na (kumbukeni) Mwenyezi Mungu atakaposema: "Ewe Isa bin Maryamu! Je, wewe uliwaambia watu: 'Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu'?" Aseme (Nabii Isa): "Wewe umetakasika na kuwa na mshirika. Hainijuzii mimi kusema ambayo si haki

وَإِذْ أَوْحَيْتُ إِلَى الْحَوَارِيِّينَ أَنْ آمِنُوا بِي وَبِرَسُولِي ۚ
قَالُوا آمَنَّا وَاشْهَدْ بِأَنَّنَا مُسْلِمُونَ ﴿١١١﴾

إِذْ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ
يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَنْ يُنَزِّلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ ۖ
قَالَ اتَّقُوا اللَّهَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾

قَالُوا نُرِيدُ أَنْ نَأْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوبُنَا وَ
نَعْلَمَ أَنْ قَدْ صَدَقْتَنَا وَنَكُونَ عَلَيْهَا
مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿١١٣﴾

قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزِلْ عَلَيْنَا
مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِأَوَّلِنَا
وَآخِرِنَا وَآيَةً مِنْكَ ۖ وَارْزُقْنَا وَأَنْتَ
خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿١١٤﴾

قَالَ اللَّهُ إِنِّي مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ ۖ فَمَنْ يَكْفُرْ بَعْدُ
مِنْكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا لَا أُعَذِّبُهُ أَحَدًا
مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿١١٥﴾

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنْتَ قُلْتَ
لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۖ قَالَ
سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ ۚ إِنْ

---

Na watu hao inataka wawe Waislamu maadamu mahala hapo pana Waislamu. Ama ikiwa hapana Waislamu basi anaweza kuwausia wasiokuwa Waislamu

Khalafu wale warithi wakiwa na shaka kuu ya maneno ya mawasii wale, wanaweza kwenda kwa hakimu kumuhadithia. Na hakimu atawaambia wale mawasii wale yamini kuthubutisha kuwa hayo waliyoyasema ni kweli. Wakitokubali yamini utabadilika wasia huo. Na wakikubali, wakaapa, utathubuti.

Na juu ya kuthibiti kwake wasia huo kwa yamini zao hizo; lakini ikidhihiri kwa dalili zisizokuwa na shaka kuwa waongo tu mawasii hao basi. Hakimu atawapa ruhusa wale warithi wale yamini ya kusema kuwa mawasii hao waongo. Basi utabadilika ule wasia.

Maelezo yao juu ya hii Aya waliyoifanya ya 107 tumeyarejeza katika Aya 282 ya *Suratul Baqarah.*

109-115. Hapa yanatajwa baadhi ya mambo yatakayotokea siku ya Kiyama. Miongoni mwa hayo ni (a) Kuulizwa Mitume habari za uma zao na (b) Kukumbushwa Nabii Isa baadhi ya neema alizopewa na Mwenyezi Mungu na (c) Kukumbushwa baadhi ya mambo waliyoyasema na waliyoyafanya wanafunzi wake (Masahaba zake).

110. Katika maelezo ya Aya makadiyani walioifanya ni ya 111 wamewataka watu warejelee Aya makhsusi za Sura makhsusi walizozitaja hapo ili waone zaidi mkorogo wao walioukoroga katika kufasiri Aya hizo. Majibu ya maelezo yao ya 2:57, 2:88 yamo katika majibizo ya *Suratul Baqarah.* Na majibu ya maelezo yao ya 2:254; 3:47; 3:50; 3:56; yamo katika Marejezo ya Juzuu ya *Tilkar Rusul.* Na majibu ya maelezo yao ya 4:158 yamo katika marejezo ya *La Yuhibb.*

كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۚ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾

yangu (kuyasema, kwa kuwa ni ya uwongo). Kama ningalisema bila shaka ungalijua; unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyo nafsini mwako; hakika Wewe ndiye ujuaye mambo ya ghaibu."

مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۖ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنتَ أَنتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾

117. "Sikuwaambia lo lote ila yale uliyoniamrisha: ya kwamba 'Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu.' Na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao; na uliponikamilisha muda wangu, Wewe ukawa mchungaji juu yao, na Wewe shahidi juu ya kila kitu."

إِن تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ ۖ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾

118. "Ikiwa utawaadhibu, basi bila shaka hao ni waja wako; na ukiwasamehe basi kwa hakika wewe ndiye Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima; (hutaambiwa kuwa wamekushinda kuwatia adabu)."

قَالَ اللَّهُ هَٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ الصَّادِقِينَ صِدْقُهُمْ ۚ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

119. Mwenyezi Mungu atasema: "Hii ndiyo Siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mbele yake mito. Humo watakaa milele. Mwenyezi Mungu amewawia (amewapa) radhi; nao wawe radhi naye. Huku ndiko kufaulu kukubwa.

لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٢٠﴾

120. Ni wa Mwenyezi Mungu tu ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo humo vyote. Naye ni Mweza juu ya kila kitu.

---

114. Makadiyani katika Aya waliyoifanya ya 115 wanakataa kuwa chakula kiliteremshwa kutoka mbinguni— au kilitaka kuletwa kutoka mbinguni; halafu kisiletwe kwa kuwa wenyewe waombaji walisema basi. Na hali ya kuwa hizi ndizo kauli mbili zinazosemwa na wafasiri hao waliowataja na wengineo, kama ilivyo katika sahifa 54 ya Juzuu ya 7 ya *Ruuhul Maany;* kama wanavyojua, ila wanajitia pambani tu kama dasturi yao; wakaandika hapa: "Maneno haya yanaonyesha ya kuwa wanafunzi wa Nabii Isa hawakuomba chakula cha mara moja, bali chakula kisichokwisha, kinachopatikana bila taabu. Aya hizo sio muradi wao ya kuwa chakula kiliteremka kutoka mbinguni." Waongo. Hapana mfasiri yo yote aliyefasiri hivi walivyofasiri wao; ila wengine wamesema kulidumu muda mrefu huko kuletwa kwao. Na tafsiri yao hii inapinga dhahir shahir hayo maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo hapa katika Aya hizi. Lakini hawamwogopi Mwenyezi Mungu kumharibia maneno Yake, kama wasivyojali pia kuyaharibu maneno ya Mtume wake na ya wanavyuoni wake; wao lao ni kutaka kuupoteza uma tu.

115. Hapa wametia maneno ya kutaka kuthubutisha uwongo wao. Wakataja natija za Vita vya 1914-1918 na vya 1939-1945. Vita hivyo havikufanya taathira yake mbaya juu ya Wakristo tu; imefanya juu ya ulimwengu mzima. Wala malipo hayo yasingezuiliwa yasije mpaka kikapita kiasi cha miaka 2000; na hapa katika wakati huu ndio yalipwe mara mbili mfululizo! Wanayatilia farumu tu hayo maneno yao yanayopepesuka huku na huku — mrama moja kwa moja.

117. Makadiyani katika Aya waliyoifanya kuwa ni ya 118 wamefasiri makusudi hivi: "Uliponifisha. . . . ." kuonyesha kuwa Nabii Isa kafa. Na tumeisema habari hii kwa urefu katika Aya ya 56 ya *Surati Aali Imran* Juzuu ya *Tilkar Rusul.* Na tukataja humo kuwa wanavyuoni wanasema kuwa tamko la *Tawaffaa* sio maana yake ya asili "kutoa roho"; na wao wanajua; basi tu. Hata katika Aya hii katika sahifa 60 ya Juzuu ya 7 ya Ruuhul Maany, ameandika huyu mwenye *Ruuhul Maany* ambaye wanajidai wamemfuata; ameandika: *"Falammaa Tawaffaytany = qabadhtany Bir Raf-i Ilas Samaa"* (Uliponichukua kwa kunipeleka mbinguni).

Si hii tafsiri ya mwenye *Ruuhul Maany* na wengine! Tena akazidi kulifasiri hili tamko la *Tawaffaytany,* akasema: *"Yuqaalu Tawaffaytul Maala = Qabadhtuhuu";* yaani tamko la *Tawaffaytu* katika asili ya lugha ya Kiarabu ni kutekeleza, kama hivi unavyosema *"Tawaffaytul Maala"* yaani nimemtekelezea mali. Si hii hizaya inazidi kuwafika hao?

119. Kuonyesha kuwa litakalomfaa mtu siku ya Kiyama ni ukweli katika Uislamu wake. Kutekeleza kama alivyoamrishwa, si Uislamu jina tu.

اٰياتها ١٦٥ (٦) سورة الانعام مكية (٥٥) ركوعاتها ٢٠

*Ina Aya 165* **SURAT AL AN-AM** *Ina Makara 20*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Sifa zote njema zinamthubutikia Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi, na akafanya giza na nuru. Na juu ya haya wale waliokufuru wanamsawazisha Mola wao (na vijiungu vya uwongo).

الحمد لله الذي خلق السموت والارض وجعل
الظلمت والنور ثم الذين كفروا بربهم يعدلون ①

2. Yeye ndiye aliyekuumbeni kwa udongo, kisha akaweka muda (wa ajali ya kila kiumbe). Na muda huo maalumu (uliowekwa kuondoka ulimwengu) uko Kwake. Juu ya haya mnafanya shaka.

هو الذي خلقكم من طين ثم قضى اجلا و
اجل مسمى عنده ثم انتم تمترون ②

3. Na yeye ndiye Mwenyezi Mungu katika mbingu na katika ardhi; anaijua ndani yenu na nje yenu; na anayajua (yote) mnayoyachuma.

وهو الله في السموت وفي الارض يعلم سركم
وجهركم ويعلم ما تكسبون ③

4. Na haiwafikii hoja yo yote katika hoja za Mola wao ila wanaikengeuka.

وما تأتيهم من اية من ايت ربهم الا كانوا
عنها معرضين ④

5. Wameikadhibisha haki ilipowafikia; kwa hivi zitawafikia habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

فقد كذبوا بالحق لما جاءهم فسوف
يأتيهم انبؤا ما كانوا به يستهزءون ⑤

6. Je, hawaoni uma ngapi tulizoziangamiza kabla yao? Tuliwamakinisha katika nchi tusivyokumakinisheni (nyinyi), na tukawapelekea mvua iendeleayo, (wakastarehe kwa kila namna ya mazao), na tukaifanya mito inapita mbele yao. Kisha tukawaangamiza kwa sababu ya dhambi zao; na tukaumba baada yao uma nyingine.

الم يروا كم اهلكنا من قبلهم من قرن مكنهم
في الارض ما لم نمكن لكم وارسلنا السماء
عليهم مدرارا وجعلنا الانهر تجري من
تحتهم فاهلكنهم بذنوبهم وانشانا من
بعدهم قرنا اخرين ⑥

7. Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi (kama walivyotaka) na wakayagusa (maandishi hayo) kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangalisema: "Haya si cho chote ila ni uchawi dhahiri (Kiini macho tu hiki; si maandishi)."

ولو نزلنا عليك كتبا في قرطاس فلمسوه
بايديهم لقال الذين كفروا ان هذا الا سحر
مبين ⑦

8. Na husema: "Mbona hakuteremshiwa Malaika (wa kutwambia kuwa kweli huyu ni Mtume)?" Na kama tungeliteremsha Malaika, (na juu ya hivi wakakataa), bila shaka shauri (yao ya

وقالوا لولا انزل عليه ملك ولو انزلنا ملكا

7. Makafiri walimwambia Mtume 'Hatukuamini kuwa wewe ni Mtume mpaka upande mbinguni, mikono mitupu na sisi tunakuona; kisha urejee, na sisi tunakuona, hali ya kuwa una daftari ambalo ndani yake muna shahada ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu."

لَقُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنْظَرُونَ ⑧

kuangamizwa) ingekatwa (mara moja, kisha wasingelipewa nafasi (muhula).

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ مَلَكًا لَجَعَلْنَاهُ رَجُلًا وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِمْ مَا يَلْبِسُونَ ⑨

9. Na kama (Mtume) tungalimfanya Malaika bila shaka tungalimfanya (kwa sura za) binadamu. (Na lau tungaliteremsha Malaika wa kushuhudia pia tungelimteremsha kwa sura za binadamu) na tungeliwatatanishia yale wanayoyatatanisha.

وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِنْ قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ⑩ ع

10. Na hakika walifanyiwa stihzai Mitume (wote) kabla yako, lakini (mwisho) yakawazunguka wale waliofanya mzaha, miongoni mwao, yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ ثُمَّ انْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ⑪

11. Sema: "Safirini katika nchi, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wakadhibishaji."

قُلْ لِمَنْ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ قُلْ لِلَّهِ ۚ كَتَبَ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۚ لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ ۚ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ⑫

12. Sema (uwaulize): "Ni vya nani vilivyomo mbinguni na ardhini?" Useme (tena kujibu): "Ni vya Mwenyezi Mungu." Yeye amejilazimisha kuwafanyia rehema (waja wake); (kwa hivyo huwapa muda, hawatesi upesi. Na pengine hawatesi mpaka Kiama au hawatesi kabisa). Hakika atakukusanyeni siku ya Kiyama, siku isiyo na shaka. Wale waliojitia khasarani hawaiamini (siku hiyo).

وَلَهُ مَا سَكَنَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ ۚ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ⑬

13. Na ni vyake (Mwenyezi Mungu vyote) vinavyotulia (na vinavyotaharaki) katika usiku na (katika) mchana; naye ndiye asikiaye na ajuaye.

قُلْ أَغَيْرَ اللَّهِ أَتَّخِذُ وَلِيًّا فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ ۗ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَسْلَمَ ۖ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ⑭

14. Sema: "Je, nifanye Mola (wangu) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, (ambaye ndiye) mwumba wa mbingu na ardhi; naye hulisha wala halishwi?" Sema: "Hakika mimi nimeamrishwa niwe wa kwanza katika wenye kusilimu na (nikaambiwa): "Usiwe miongoni mwa wanaomshirikisha (Mwenyezi Mungu)."

قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ⑮

15. Sema: "Mimi naogopa adhabu ya Siku kubwa (hiyo) ikiwa nitamuasi Mola wangu."

مَنْ يُصْرَفْ عَنْهُ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمَهُ ۚ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ ⑯

16. Atakayeepushwa nayo (adhabu hiyo) Siku hiyo (ya Kiyama), bila shaka amemrehemu (Mwenyezi Mungu); na huku ndiko kufaulu kuliko dhahiri.

---

12. Kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu Ana rehema kubwa kabisa juu ya wanaadamu. Amewaumba kwa kuwapa (a) roho na (b) vingine Asivyowapa viumbe vyengine na (c) utambuzi na (d) akili na (e) kujua kusema na (f) kujua kuandika na (g) kujua kusoma na . . . Na juu ya hivi Akawaletea na Mitume wa kuzidi kuwafumbua macho. Na Amewawekea jaza ya Pepo hao watakaofuata. Basi wasiokubali kutengenea—juu ya yote haya—wamejitia khasarani wenyewe.

14. Hapa wanazinduliwa wale wanaoacha kumwabudu Mwenyezi Mungu Ambaye baadhi ya sifa Zake ni hiyo, iliyo katika Aya ya 13, wakaomba mizimu na mapango na makaburi na mapepo. Yana jambo gani hayo mapepo na makaburi na mapango na mizimu? Si upotofu wa akili tu huo? Bali na ukafiri pia kuwaomba: "Bwana! Nimekuja naomba unipe . . ." Mwislamu kamili hasubutu kusema hivi. Kufanya hivyo ni namna ya

17. Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara (taabu), basi hakuna yo yote awezaye kuyaondoa ila Yeye; na kama akikugusisha kheri (hakuna wa kuweza kuondoa ila Yeye tu peke yake). Yeye ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu.

وَإِن يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۖ
وَإِن يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾

18. Naye ni Mshindaji (amewatawala) waja wake (wote); naye ndiye Mwenye hikima na Mwenye khabari zote.

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۚ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿١٨﴾

19. Sema (uwaulize): "Kitu gani ushahidi wake ndio mkubwa zaidi?" Kisha sema: (ujibu) "Mwenyezi Mungu. (Basi Yeye ndiye) shahidi baina yangu na baina yenu. Na Qurani hii imefunuliwa kwangu ili kwa hiyo nikuonyeni nyinyi na kila imfikiayo. Je, kwa yakini nyinyi mnashuhudia ya kwamba wako waungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu?" Sema (tena); "Mimi sishuhudii." Useme (tena vile vile) "Yeye ni Mungu mmoja tu. Na hakika mimi ni mbali na hao mnaowashirikisha (na Mwenyezi Mungu)."

قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ شَهَادَةً ۖ قُلِ اللَّهُ ۖ شَهِيدٌ
بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۚ وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَٰذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُم
بِهِ وَمَن بَلَغَ ۚ أَئِنَّكُمْ لَتَشْهَدُونَ أَنَّ مَعَ اللَّهِ
آلِهَةً أُخْرَىٰ ۚ قُل لَّا أَشْهَدُ ۚ قُلْ إِنَّمَا هُوَ إِلَٰهٌ
وَاحِدٌ وَإِنَّنِي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿١٩﴾

20. Wale tuliowapa Kitabu wanayafahamu haya kama wanavyowafahamu watoto wao. Wale wanaojitia khasarani (miongoni mwao) ndio hawaamini.

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ
أَبْنَاءَهُمُ ۘ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا
يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾

21. Na nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye uwongo Mwenyezi Mungu au azikadhibishaye hoja Zake? Hakika madhalimu hawatafaulu.

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ
بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٢١﴾

22. Na (wakumbushe) siku ambayo tutawakusanya wote pamoja, kisha tutawaambia wale walioshirikisha: "Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai (kuwa hao washirika wa Mungu)"

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا أَيْنَ
شُرَكَاؤُكُمُ الَّذِينَ كُنتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٢٢﴾

23. Kisha hautakuwa udhuru wao isipokuwa kusema: "Wallahi, Mola wetu! Hatukuwa washirikina." (Ati wanamdanganya Mwenyezi Mungu).

ثُمَّ لَمْ تَكُن فِتْنَتُهُمْ إِلَّا أَن قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا
كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٢٣﴾

24. Angalia jinsi wanavyosema uwongo juu ya nafsi zao. Na yamewapotea waliyokuwa wakiyazua (ya kuwa waungu wao hao watawaombea mbele ya Mwenyezi Mungu).

انظُرْ كَيْفَ كَذَبُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ ۚ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا
كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٤﴾

25. Na wako miongoni mwao wanaokusikiliza, na (kama kwamba) tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu (hayo wanayoyasikia), na (kama

وَمِنْهُم مَّن يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ ۖ وَجَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ
أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۚ وَإِن يَرَوْا

---

ushirikina. Basi natujiepushe na chembe hii ya ushirikina.

17-18. Zinazidi kubainisha kuwa wa kuombwa na kutegemewa ni Mwenyezi Mungu tu Peke Yake kwani hakuna wa kupitisha Alitakalo ila Yeye.

19. Makafiri wakimwambia Mtume 'Wewe si Mtume', kama tulivyoona na tutavyoona katika Aya nyingi. Basi anaambiwa Mtume asijali kukataliwa na wao maadamu Mwenyezi Mungu Mwenyewe Anamkiri kuwa ni Mtume Wake.

kwamba) pana uziwi masikioni mwao; na wakiziona kila hoja hawaziamini. Hata wanapokujia kukujadili, wale waliokufuru husema: "Hizi (unazozisoma) si cho chote ila ni hadithi tu za watu wa kale."

كُلَّ ءَايَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوكَ
يُجَٰدِلُونَكَ يَقُولُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا إِنْ هَٰذَآ إِلَّآ
أَسَٰطِيرُ ٱلْأَوَّلِينَ ﴿٢٥﴾

26. Nao wanakataza (watu kuyafuata) haya; na (wenyewe) wanajiweka mbali nayo; nao hawaangamizi ila nafsi zao; hali hawatambui (wenyewe kuwa wanaangamiza nafsi zao. Wao wamo furahani tu kuwa wanampinga Nabii Muhammad).

وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْـَٔوْنَ عَنْهُ وَإِن يُهْلِكُونَ
إِلَّآ أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٦﴾

27. Na ungeona (Siku ya Kiama) watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema "Laiti tungerudishwa (ulimwenguni); wala hatutakadhibisha (tena) Aya za Mola wetu, na tutakuwa katika wanaoamini"; (ungewaona siku hiyo namna wanavyodahadari).

وَلَوْ تَرَىٰٓ إِذْ وُقِفُوا عَلَى ٱلنَّارِ فَقَالُوا يَٰلَيْتَنَا نُرَدُّ
وَلَا نُكَذِّبَ بِـَٔايَٰتِ رَبِّنَا وَنَكُونَ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٧﴾

28. (Siyo. Hawatatenda mema yo yote). Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila shaka wangeyarudia yale waliyokatazwa; na bila shaka hao ni waongo (tu).

بَلْ بَدَا لَهُم مَّا كَانُوا يُخْفُونَ مِن قَبْلُ وَلَوْ رُدُّوا
لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَٰذِبُونَ ﴿٢٨﴾

29. Na walisema: "Hakuna mengine ila maisha yetu (haya tu) ya dunia, wala sisi hatutafufuliwa."

وَقَالُوٓا إِنْ هِىَ إِلَّا حَيَاتُنَا ٱلدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ
بِمَبْعُوثِينَ ﴿٢٩﴾

30. Na ungeona (Siku ya Kiama) watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, akawaambia: "Je, si kweli haya?" Na wao wakasema: "Kwa nini? (Ni haki Wallahi), tunaapa kwa jina la Mola wetu." Aseme (Mwenyezi Mungu): "Basi ionjeni adhabu kwa sababu ya kule kukanusha kwenu."

وَلَوْ تَرَىٰٓ إِذْ وُقِفُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ قَالَ أَلَيْسَ هَٰذَا
بِٱلْحَقِّ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا ٱلْعَذَابَ بِمَا
كُنتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٠﴾ ع

31. Bila shaka wamekwishapata khasara wale waliokadhibisha kukutana na (Jaza ya) Mwenyezi Mungu; hata ilipowafikia kwa ghafla saa ile (ya kukata roho), walisema: "Oo! Majuto yetu juu ya yale tuliyoyapuza." Nao watabeba mizigo (ya madhambi) yao migongoni mwao. Angalieni. Ni mabaya mno wanayoyabeba.

قَدْ خَسِرَ ٱلَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَآءِ ٱللَّهِ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَتْهُمُ
ٱلسَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوا يَٰحَسْرَتَنَا عَلَىٰ مَا فَرَّطْنَا فِيهَا
وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُمْ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ أَلَا سَآءَ
مَا يَزِرُونَ ﴿٣١﴾

32. Na maisha ya dunia (hii) si kitu ila mchezo tu na upuzi. Na bila shaka nyumba ya Akhera ni bora zaidi (bila kiasi kuliko hii dunia) kwa wale wamchao (Mwenyezi Mungu). Basi hamtii akilini (haya mnayoambiwa)?

وَمَا ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَآ إِلَّا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَلَلدَّارُ
ٱلْءَاخِرَةُ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ يَتَّقُونَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٣٢﴾

---

26. Inabainishwa hapa kuwa hao wanaujua ukweli wa dini ya Kiislamu—lakini wanaipinga tu na kuwazuilia watu kuifuata—wanajiangamiza wenyewe.

29. Wanajitia nguvu wenyewe katika kufanya mabaya—na wanawatia nguvu wengine—kwa kuwaambia: "Hakuna kufufuliwa wala kulipwa, natufanye tunayoyataka tunavyopenda."

30-31. Yanatajwa baadhi ya yatakayowafika waovu.

33. Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha yale wanayoyasema (katika kukutukana na kukukadhibisha). Basi wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu hao wanakanusha hoja za Mwenyezi Mungu, (Mungu atawalipa).

قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ فَإِنَّهُمْ
لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ
يَجْحَدُونَ ﴿٣٣﴾

34. Na hakika walikadhibishwa Mitume (wote) kabla yako, wakavumilia kwa kule kukadhibishwa na kuudhiwa mpaka ikawafikia nusura yetu. Na hakuna abadilishaye maneno ya (waadi wa) Mwenyezi Mungu. Na bila shaka zimekufikia khabari za Mitume hao.

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا
كُذِّبُوا وَأُوذُوا حَتَّىٰ أَتَاهُمْ نَصْرُنَا ۚ وَلَا مُبَدِّلَ
لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۚ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِن نَّبَإِ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٤﴾

35. Na ikiwa ni makubwa kwako huku kujitenga kwao (na haya unayowaambia kwa kuwa wanataka waonyeshwe hiyo miujiza wanayoitaka; ukawa unataka sharti waonyeshwe miujiza hiyo, na Mimi sitaki), basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini katika ardhi (kwenda kutafuta miujiza hiyo) au (unaweza kupata) ngazi ukapanda mbinguni na kuwaletea miujiza (wanayoitaka, fanya). Na kama Mwenyezi Mungu angependa bila shaka angewakusanya katika uwongozi (huu kwa miujiza hiyo; lakini hataki). Basi usiwe miongoni mwa wasiojua.

وَإِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكَ إِعْرَاضُهُمْ فَإِنِ اسْتَطَعْتَ
أَن تَبْتَغِيَ نَفَقًا فِي الْأَرْضِ أَوْ سُلَّمًا فِي السَّمَاءِ
فَتَأْتِيَهُم بِآيَةٍ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى
الْهُدَىٰ ۚ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٣٥﴾

36. Wanaokubali ni wale wanaosikia. Na (ama) watu (hawa) wasiotaka kusikia cho chote Mwenyezi Mungu atawafufua (makafiri), kisha watarejeshwa kwake.

إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ ۘ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ
اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٣٦﴾

37. Na husema: "Kwa nini hakuteremshiwa miujiza (tunayoitaka) kutoka kwa Mola wake?" Sema: "Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza wa kuteremsha miujiza;" lakini wengi wao hawajui (sababu ya kutoletwa miujiza waitakayo).

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ ۚ قُلْ إِنَّ اللَّهَ
قَادِرٌ عَلَىٰ أَن يُنَزِّلَ آيَةً وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ
لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾

38. Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake mbili. ila ni umati

وَمَا مِن دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ

---

33. Mtume alikuwa ni binaadamu anayehisi upesi mema na mabaya, kwa hivi akihuzunika sana kuona watu hawafuati yale mazuri anayowaambia wala hawakubali kuwacha yale mabaya anayowakataza. Na akihuzunika kwa kule kukadhibishwa, na hali ya kuwa wanamjua kuwa si mwongo. Basi Mwenyezi Mungu ndio Anamwambia: "Hawa makafiri wanakujua kuwa wewe si mwongo lakini hawayataki tu haya uliyokuja nayo ambayo yatawaondoshea mabaya yao waliyoyazowea." Mzowea ya kunyonga, ya kuchinja haiwezi.

Na anabainishiwa katika Aya ya 34 kuwa hayo yanayomfika yeye ndiyo yaliyowafika Mitume wengine.

35. Nabii Muhammad (s.a.w.) alikuwa na hamu kubwa kabisa ya kutaka watu wote wasilimu upesi upesi. Wapewe hiyo miujiza wanayoitaka wishe udhia. Lakini Mwenyezi Mungu alikuwa hapendi Uislamu huo. Akipenda wasilimu baada ya kuyafahamu vyema hayo wanayoambiwa. Siyo wanasilimu kwa nguvu za miujiza, kama alivyobainisha haya katika Aya ya 51 *Suratul Ankabut* na nyinginezo kama hiyo ya 37 inayokuja.

Aya hii waliyoifanya ni ya 36 wameikoroga kabisa. Na yote ni kwa ajili ya kukimbia kutaja miujiza. Basi isome tafsiri yake na maelezo yake katika hii tafsiri yetu na tafsiri zo zote zilizomo ulimwenguni zisizokuwa zao.

38. Kuonyesha kuwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu Umeenea kila kitu na Unaendesha vilivyo kila kitu. Hapana

kama nyinyi (tunadhibiti kila walifanyalo). Hatukupuza Kitabuni (mwetu) kitu cho chote. Kisha watakusanywa kwa Mola wao (awalipe).

إِلَّآ أُمَمٌ أَمْثَالُكُم ۚ مَّا فَرَّطْنَا فِى ٱلْكِتَٰبِ مِن شَىْءٍ ۚ
ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ ﴿٣٨﴾

39. Na wale waliokadhibisha hoja zetu ni viziwi na mabubwi na wamo gizani. Amtakaye Mwenyezi Mungu humwachia kupotea; na amtakaye humweka katika njia iliyonyoka.

وَٱلَّذِينَ كَذَّبُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا صُمٌّ وَبُكْمٌ فِى ٱلظُّلُمَٰتِ ۗ
مَن يَشَإِ ٱللَّهُ يُضْلِلْهُ وَمَن يَشَأْ يَجْعَلْهُ عَلَىٰ
صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٣٩﴾

40. Sema: "Niambieni, kama ikikufikieni adhabu ya Mwenyezi Mungu (ya hapa duniani) au ikikufikieni ile saa (ya kufikwa na adhabu ya Akhera) je, mtamwita asiyekuwa Mwenyezi Mungu (akuondosheeni) ikiwa nyinyi ni wakweli?"

قُلْ أَرَءَيْتَكُمْ إِنْ أَتَىٰكُمْ عَذَابُ ٱللَّهِ أَوْ أَتَتْكُمُ ٱلسَّاعَةُ
أَغَيْرَ ٱللَّهِ تَدْعُونَ إِن كُنتُمْ صَٰدِقِينَ ﴿٤٠﴾

41. Bali yeye ndiye mtakayemwomba, naye atakuondoleeni mnayomwomba (kukuondosheeni) akipenda. (Nayo ni yale ya kiduniani si ya Kiakhera), na mtasahau mnaowashirikisha (na Mwenyezi Mungu).

بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ
إِن شَآءَ وَتَنسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ ﴿٤١﴾

42. Na kwa yakini tulipeleka (Mitume) kwa uma zilizokuwa kabla yako, kisha tukazitia katika dhiki na mashaka ili zipate kunyenyekea (baada ya kufanya ukaidi).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَآ إِلَىٰٓ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَخَذْنَٰهُم
بِٱلْبَأْسَآءِ وَٱلضَّرَّآءِ لَعَلَّهُمْ يَتَضَرَّعُونَ ﴿٤٢﴾

43. Kwa nini wasinyenyekee ilipowafikia adhabu yetu? Walakini nyoyo zao zilikuwa ngumu, na Shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya.

فَلَوْلَآ إِذْ جَآءَهُم بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا۟ وَلَٰكِن قَسَتْ
قُلُوبُهُمْ وَزَيَّنَ لَهُمُ ٱلشَّيْطَٰنُ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾

44. Basi walipopuza yale waliyokuwa wakikumbushwa tuliwafungulia milango ya kila kitu (walichokuwa wakikitaka). Mpaka walipofurahia yale waliyopewa, hapo tuliwakamata kwa ghafla; na mara wakawa wenye kukata tamaa.

فَلَمَّا نَسُوا۟ مَا ذُكِّرُوا۟ بِهِۦ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ أَبْوَٰبَ كُلِّ
شَىْءٍ حَتَّىٰٓ إِذَا فَرِحُوا۟ بِمَآ أُوتُوٓا۟ أَخَذْنَٰهُم بَغْتَةً فَإِذَا
هُم مُّبْلِسُونَ ﴿٤٤﴾

45. Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu (wakaondoka ulimwenguni). Na sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Muumba wa walimwengu (wote).

فَقُطِعَ دَابِرُ ٱلْقَوْمِ ٱلَّذِينَ ظَلَمُوا۟ ۚ وَٱلْحَمْدُ لِلَّهِ
رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٤٥﴾

46. Sema: "Niambieni kama Mwenyezi Mungu akikuondoleeni kusikia kwenu na kuona kwenu, na akazipiga muhuri nyoyo zenu (kisiingie kitu cho

قُلْ أَرَءَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ ٱللَّهُ سَمْعَكُمْ وَأَبْصَٰرَكُمْ
وَخَتَمَ عَلَىٰ قُلُوبِكُم

---

kinachokwenda ovyo ovyo (kinakwenda *naturally* tu), Hapana. Vinaendeshwa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu kwa Mpango Madhubuti.

40-41. Haya yanaonyesha kuwa makafiri wa zama hizo walikuwa afadhali—katika itikadi yao juu ya Uweza wa Mwenyezi Mungu—kuliko hawa Waislamu wa zama hizi wanaoomba Mizimu na Makaburi na Majini na. . . Huwa kila ikishitadi balaa ndipo wanaposhitadi kuwaomba hao wakamwacha Mwenyezi Mungu. Kupotea kukubwa kabisa!

43. Kuonyesha huruma ya Mwenyezi Mungu juu ya viumbe Vyake, hata wakimwasi vipi wakirejea Atawapokea.

44. Kuwahadharisha wabaya kuwa wasione tamu wakiona wanapururiwa (wanapuliziwa) tu neema juu ya uovu wao; watatiwa tu mkononi siku moja.

46. Wanaonyeshwa kuwa neema zote Mwenyewe Mwenyezi Mungu, sio hao waola wao wasioweza hata kujivutia nguo.

مَنْ إِلَٰهٌ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُم بِهِ ۗ انظُرْ كَيْفَ
نُصَرِّفُ الْآيَاتِ ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُونَ ﴿٤٦﴾

chote cha kheri), ni nani mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu awezaye kukuleteeni tena? Tazama jinsi tunavyoeleza Aya, kisha wao wanapuza.

قُلْ أَرَأَيْتَكُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُ اللَّهِ بَغْتَةً أَوْ
جَهْرَةً هَلْ يُهْلَكُ إِلَّا الْقَوْمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤٧﴾

47. Sema: "Niambieni kama ikikufikieni kwa ghafla (kwa siri) adhabu ya Mwenyezi Mungu au (ikakufikieni) kwa dhahiri, nani watakaoangamizwa isipokuwa watu waliodhulumu?"

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۖ
فَمَنْ آمَنَ وَأَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
يَحْزَنُونَ ﴿٤٨﴾

48. Na hatutumi Mitume ila huwa watoaji khabari njema na waonyaji. Na wenye kuamini na kufanya wema haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا يَمَسُّهُمُ الْعَذَابُ بِمَا كَانُوا
يَفْسُقُونَ ﴿٤٩﴾

49. Na wale waliokadhibisha Aya zetu itawagusa (itawapata) adhabu kwa sababu ya kule kuasi kwao.

قُل لَّا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ
الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا
يُوحَىٰ إِلَيَّ ۚ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ۚ
أَفَلَا تَتَفَكَّرُونَ ﴿٥٠﴾

50. Sema: "Mimi sikwambieni kuwa ninazo khazina za Mwenyezi Mungu (nikakupeni mnayoyataka;) wala (sikukwambieni kuwa) najua mambo ya siri (ya Mwenyezi Mungu nikakubainishieni yatakayokufikieni katika biashara zenu na mengineyo kama mlivyotaka nikwambieni), wala sikwambieni kuwa Mimi ni Malaika (hata mkanambia: 'kwa nini unakula na kuoa'). Mimi sifuati ila yale yaliyofunuliwa kwangu." Sema: "Je, kipofu na mwenye macho huwa sawa? Basi je, hamfikiri?"

وَأَنذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَن يُحْشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ ۙ
لَيْسَ لَهُم مِّن دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَّعَلَّهُمْ
يَتَّقُونَ ﴿٥١﴾

51. Na uwaonye kwa (Qurani) hii wale wanaoogopa ya kwamba watakusanywa kwa Mola wao, hali kuwa hawana mlinzi yo yote, isipokuwa yeye, wala mwombezi. (Waonye hivi) ili wapate kumcha.

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِالْغَدَاةِ
وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۖ مَا عَلَيْكَ مِنْ
حِسَابِهِم مِّن شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِم مِّن
شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٥٢﴾

52. Wala usiwafukuze wale wanaomwabudu Mola wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi yake. Si juu yako hisabu yao hata kidogo wala hisabu yako si juu yao hata kidogo, hata uwafukuze. (Ukiwafukuza) utakuwa miongoni mwa madhalimu.

---

50. Makafiri walimwambia kama kweli yeye Mtume basi naawape hiki na hiki . . . na awajulishe kabla ya kuondoka kwa safari zao za biashara kuwa, safari hii litawafika hili na watapata hivi . . . na wakamwambia kwa nini anakula na anaoa . . .

Basi ndio wakajibiwa kwa haya yaliyotajwa katika Aya hii.

*N.B.*—Na hapa Mtume anaambiwa kuwa hajui *Ilmul-Ghaaybi;* na wapiga bao wanasema kuwa wao wanajua. Waongo wakubwa.

52. Watu Wakubwa wa Kikureshi katika kutafuta udhuru tu wa kutomfuata Mtume—walimwambia Mtume 'Sisi hatuwezi kuingia katika dini hii tukawa sawa sawa na watumwa hawa na mafakiri hawa waliokufuata ukawafanya sawa sawa na bwana zao, na sawa sawa na mabwana wengine watukufu. Ukitaka tukufuate wafukuze hawa wasije tena kwako (au wawekee siku yao makhsusi na mahala pao makhsusi), hapo tutakufuata. Akaambiwa Mtume na Mwenyezi Mungu maneno haya na akambainishia kuwa kila mtu ana hisabu yake — mbaya

53. Na namna hii tumewafanyia mtihani baadhi yao (viumbe, yaani matajiri) kwa baadhi (yao wengine walio mafakiri) ili waseme (walio matajiri): "Je, hao ndio Mwenyezi Mungu amewafanyia ihisani miongoni mwetu (pasina kutufanyia sisi? Uwongo huo, si dini ya haki hiyo kama wameijua wao kabla yetu." Basi Mwenyezi Mungu akasema): "Je, Mwenyezi Mungu hawajui wanaomshukuru?"

وَكَذَٰلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهَٰؤُلَاءِ
مَنَّ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ بَيْنِنَا ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ
بِالشَّاكِرِينَ ﴿٥٣﴾

54. Na (wewe Mtume) wanapofika wale (mafakiri) wanaoamini Aya zetu (na hali wamekosa kidogo; wanakuja kutubia) waambie "Amani iwe juu yenu, Mola wenu amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akafanya wema, kuwa Mwenyezi Mungu atamghufiria kwani yeye ni Mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa rehema.

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ
عَلَيْكُمْ ۖ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۖ أَنَّهُ
مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِنْ بَعْدِهِ
وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٤﴾

55. Na namna hii tunazieleza Aya (ili idhihiri haki), na ili njia ya waovu ibainike.

وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ وَلِتَسْتَبِينَ سَبِيلُ
الْمُجْرِمِينَ ﴿٥٥﴾ ع

56. Sema: "Mimi nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu (peke yake)." Sema: "Sifuati matamanio yenu, maana hapo nitapotea na sitakuwa miongoni mwa walioongoka."

قُلْ إِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ
اللَّهِ ۚ قُلْ لَا أَتَّبِعُ أَهْوَاءَكُمْ ۙ قَدْ ضَلَلْتُ إِذًا وَمَا
أَنَا مِنَ الْمُهْتَدِينَ ﴿٥٦﴾

57. Sema: "Mimi ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu (ya ukweli wa haya niliyo nayo); nanyi mmeikadhibisha, basi mimi sina (hiyo adhabu) mnayoitaka kwa haraka. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Anahadithia yaliyo kweli; naye ni bora kuliko wote wanaohukumu."

قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِنْ رَبِّي وَكَذَّبْتُمْ بِهِ ۚ
مَا عِنْدِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ ۚ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ ۖ
يَقُصُّ الْحَقَّ ۖ وَهُوَ خَيْرُ الْفَاصِلِينَ ﴿٥٧﴾

58. Sema: "Lau ningalikuwa nayo mnayoyataka kwa upesi, basi shauri lingalikwisha (mara moja) baina yangu na baina yenu. (Ningekuangamizeni tu kama mnavyotaka. Lakini amri haiko kwangu). Na Mwenyezi Mungu (Mwenyewe) anawajua madhalimu."

قُلْ لَوْ أَنَّ عِنْدِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ لَقُضِيَ
الْأَمْرُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِالظَّالِمِينَ ﴿٥٨﴾

59. Na ziko kwake (Mwenyezi Mungu tu) funguo za siri; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na anajua yaliyomo barani na baharini. Na halianguki jani ila analijua. Wala (haianguki) punje katika giza la ardhi (ila anaijua). Wala (hakianguki) kilichorutubika wala kilichoyabisika (ila anakijua). (Hapana cho chote), ila kimo katika Kitabu kidhihirishacho (kila jambo).

وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۚ
وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ
وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ
وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

---

hatanufaika siku ya Kiama kwa ajili ya rafiki yake mwema aliyekuwa naye duniani; na mwema hatadhurika Kiama kwa rafiki yake mbaya aliyekuwa naye duniani maadamu alikuwa akimwasa, naye hasikii.

59. Baadhi ya sifa kubwa za Mwenyezi Mungu.

60. Naye ndiye Anayekufisheni (Anayekutieni usingizi) wakati wa usiku, na Anayafahamu mnayotenda wakati wa mchana; kisha Yeye hukufufueni humo (mchana) ili muda uliowekwa (wa kuishi kwenu) umalizike. Kisha, Kwake tu (Mwenyezi Mungu) marudio yenu, Akwambieni (yote) mliyokuwa mkiyafanya.

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفّٰىكُمْ بِالَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ
بِالنَّهَارِ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضٰى أَجَلٌ
مُّسَمًّى، ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنَبِّئُكُمْ
بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٠﴾ ع ١٣

61. Naye ndiye Mwenye kushinda, aliye juu ya waja wake (wote). Na hukuleteeni (Malaika) wanaohifadhi (amali zenu—wanadhibiti kila mnayoyafanya). Hata mmoja wenu anapofikiwa na mauti, wajumbe wetu humfisha, nao hawafanyi taksiri (kosa—yaani hawakhalifu walivyoamrishwa).

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ
حَفَظَةً، حَتّٰى إِذَا جَآءَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ
رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفَرِّطُونَ ﴿٦١﴾

62. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki. Sikilizeni! Hukumu ni Yake (tu Mwenyewe Mwenyezi Mungu). Naye ni Mwepesi kuliko wote wanaohisabu.

ثُمَّ رُدُّوا إِلَى اللّٰهِ مَوْلٰىهُمُ الْحَقِّ، أَلَا لَهُ الْحُكْمُ
وَهُوَ أَسْرَعُ الْحٰسِبِينَ ﴿٦٢﴾

63. Sema: "Ni nani anayekuokoeni katika viza (taabu) vya bara na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa sauti ndogo (mkasema): "Kama akituokoa katika (baa) hii, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru."

قُلْ مَنْ يُنَجِّيكُمْ مِّنْ ظُلُمٰتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ
تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا وَّخُفْيَةً: لَئِنْ أَنْجٰنَا مِنْ هٰذِهِ
لَنَكُونَنَّ مِنَ الشّٰكِرِينَ ﴿٦٣﴾

64. Sema: "Mwenyezi Mungu hukuokoeni katika hayo na katika kila mashaka, kisha nyinyi mnamshirikisha"!

قُلِ اللّٰهُ يُنَجِّيكُمْ مِّنْهَا وَمِنْ كُلِّ كَرْبٍ ثُمَّ أَنْتُمْ
تُشْرِكُونَ ﴿٦٤﴾

65. Sema: Yeye ndiye Mwezaji wa kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au kukuvurugenivurugeni (Muwe) makundi (yasiyopatana), na (Mweza wa) kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzao." Tazama jinsi tunavyoeleza Aya (kwa namna hii) ili wapate kufahamu. (Nao hawataki kufahamu).

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلٰى أَنْ يَّبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّنْ
فَوْقِكُمْ أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعًا
وَّيُذِيقَ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ، اُنْظُرْ كَيْفَ
نُصَرِّفُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ ﴿٦٥﴾

66. Na watu wako wameikadhibisha (Qurani) hali hiyo ni haki. Sema: "Mimi si mlinzi juu yenu."

وَكَذَّبَ بِهِ قَوْمُكَ وَهُوَ الْحَقُّ، قُلْ لَّسْتُ
عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ ﴿٦٦﴾

67. Kila khabari (iliyotajwa hapa) ina wakati wake (maalumu kwa kufika). Na hivi karibuni mtajua (haya).

لِكُلِّ نَبَإٍ مُّسْتَقَرٌّ، وَّسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾

68. Na (wewe Mwislamu kama kweli Mwislamu, si munafiki) unapowaona wale wanaozungumza (kuzikadhibisha) Aya zetu, basi jitenge nao (wende zako) mpaka wazungumze

وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي اٰيٰتِنَا فَأَعْرِضْ
عَنْهُمْ حَتّٰى يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ، وَإِمَّا

---

60. Makadiyani katika hii Aya waliyoifanya ni ya 61 wamejidai kumzulia mwenye *Bahrul Muhyt*. Na sisi tumekwisha kuonyesha katika Aya ya 117 ya *Suratul Maida* na katika Aya ya *Suratul Imran* — tafsiri za wanavyuoni juu ya tamko la *Tawaffaa*.

68-70. Inatajwa namna ya kufanya unapopambana na wabaya — (a) Yapuuze wanayoyasema na (b)

يُنسِيَنَّكَ الشَّيْطَٰنُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرَىٰ مَعَ
الْقَوْمِ الظَّٰلِمِينَ ﴿٦٨﴾

maneno mengine. Na kama Shetani akikusahaulisha (ukakaa nao, na hali wamo katika mazungumzo haya), basi baada ya kutanabahi. usikae pamoja nao (hawa) watu madhalimu.

وَمَا عَلَى الَّذِينَ يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِم مِّن شَيْءٍ
وَلَٰكِن ذِكْرَىٰ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿٦٩﴾

69. Wala si juu ya wale wanaomcha (Mwenyezi Mungu) hisabu yao (hao madhalimu) hata kidogo, lakini ni (juu yao kuwapa) mauidha ili wapate kujiepusha (na mabaya yao hayo wayafanyayo).

وَذَرِ الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَعِبًا وَلَهْوًا
وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَوٰةُ الدُّنْيَا ۚ وَذَكِّرْ بِهِ أَن تُبْسَلَ
نَفْسٌ بِمَا كَسَبَتْ ۖ لَيْسَ لَهَا مِن دُونِ اللَّهِ وَلِيٌّ
وَلَا شَفِيعٌ ۚ وَإِن تَعْدِلْ كُلَّ عَدْلٍ لَّا يُؤْخَذْ
مِنْهَا ۗ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ أُبْسِلُوا بِمَا كَسَبُوا ۖ لَهُمْ شَرَابٌ
مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

70. Na waache wale walioifanya ni mchezo na upuzi dini yao (hii aliyowaletea Mwenyezi Mungu), na yamewadanganya maisha ya dunia. Basi wakumbushe kwa (hiyo Qurani watahadhari) isije (kila) nafsi (katika nafsi zao) ikaangamizwa kwa sababu ya yale iliyoyachuma. Haitakuwa na mlinzi (nafsi hiyo) wala mwombezi yo yote mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hata ikatoa fidia ya kila namna haitapokelewa. Hao ndio walioangamizwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Wao watapata kinywaji cha maji ya moto kabisa na adhabu iumizayo, kwa sababu ya kukanusha (kwao).

قُلْ أَنَدْعُوا مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا
وَنُرَدُّ عَلَىٰ أَعْقَابِنَا بَعْدَ إِذْ هَدَىٰنَا اللَّهُ كَالَّذِي
اسْتَهْوَتْهُ الشَّيَٰطِينُ فِي الْأَرْضِ حَيْرَانَ لَهُ
أَصْحَٰبٌ يَدْعُونَهُ إِلَى الْهُدَى ائْتِنَا ۗ قُلْ إِنَّ
هُدَى اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ ۖ وَأُمِرْنَا لِنُسْلِمَ لِرَبِّ
الْعَٰلَمِينَ ﴿٧١﴾

71. Sema: "Je, tuwaabudu wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatupi faida (tukiwabudu) wala hawawezi kutudhuru (tukitowaabudu), na turudishwe nyuma baada ya Mwenyezi Mungu kutuongoza, (tuwe) sawa na wale ambao mashetani wamewapoteza; wakiwayawaya katika ardhi? Wanao marafiki wanaweta katika uwongofu (wakisema): "Njooni kwetu," (na hawasikii. Hatui katika watu hao). Sema: "Uwongozi khasa ni uwongozi wa Mwenyezi Mungu, na tumeamrishwa tumnyenyekee (Yeye) Mola wa walimwengu wote."

وَأَنْ أَقِيمُوا الصَّلَوٰةَ وَاتَّقُوهُ ۚ وَهُوَ الَّذِي إِلَيْهِ
تُحْشَرُونَ ﴿٧٢﴾

72. Na (tumeambiwa) "Simamisheni Sala na mcheni Yeye, naye ndiye ambaye mtakusanywa kwake"

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَٰوَٰتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۖ
وَيَوْمَ يَقُولُ كُن فَيَكُونُ ۚ قَوْلُهُ الْحَقُّ ۚ وَلَهُ
الْمُلْكُ يَوْمَ يُنفَخُ فِي الصُّورِ ۚ عَٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَٰدَةِ ۚ
وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٧٣﴾

73. Naye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi kwa haki. Na wakati anaposema (kuliambia jambo): "Kuwa," basi huwa. Kauli yake ni haki, na ufalme ni wake siku itakapopulizwa parapanda (baragumu ya kufisha na kufufua viumbe). Mjuzi wa ya siri na ya dhahiri; naye ndiye Mwenye hikima (Mwenye kutengeneza vizuri kila lake) na Mwenye khabari zote.

وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِيمُ لِأَبِيهِ آزَرَ أَتَتَّخِذُ أَصْنَامًا

74. Na (kumbukeni) Ibrahimu alipomwambia baba yake, Azar: "Unawafanya masanamu kuwa

---

Uwakanye mpaka waache hayo. Wakitosikia (c) Ondoka.

71. Wanasimangwa wanaokubali kupotezwa na Shetani, na hali ya kuwa wanao wa kuwaongoza.

74: Hili Azar ndilo jina khasa au lakabu (jina la kupangwa) la baba yake Nabii Ibrahimu. Na yeye inaonyesha

ءَالِهَةً ۖ إِنِّىٓ أَرَىٰكَ وَقَوْمَكَ فِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٧٤﴾

waungu? Hakika ninakuona wewe na watu wako mumo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri.

وَكَذَٰلِكَ نُرِىٓ إِبْرَٰهِيمَ مَلَكُوتَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ
وَٱلْأَرْضِ وَلِيَكُونَ مِنَ ٱلْمُوقِنِينَ ﴿٧٥﴾

75. Na namna hivi tulimwonyesha Ibrahimu ufalme wa mbingu na ardhi (kuwa ni wa Mungu), na ili awe miongoni mwa wenye yakini.

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ ٱلَّيْلُ رَءَا كَوْكَبًا ۖ قَالَ هَٰذَا
رَبِّى ۖ فَلَمَّآ أَفَلَ قَالَ لَآ أُحِبُّ ٱلْءَافِلِينَ ﴿٧٦﴾

76. Na usiku ulipomwingilia (Ibrahimu na hali kakaa na makafiri), akaona nyota, alinena (makusudi kutaka kuwavuta watumie fikira zao): "(Nyota) hii ni Mola wangu." Ilipotua (ikapotea), alisema (kuwaambia wale makafiri kama kwamba yu pamoja nao katika ibada ile): "Sipendi waola wanaopotea (hawawepo ila wakati makhsusi tu)."

فَلَمَّا رَءَا ٱلْقَمَرَ بَازِغًا قَالَ هَٰذَا رَبِّى ۖ فَلَمَّآ أَفَلَ
قَالَ لَئِن لَّمْ يَهْدِنِى رَبِّى لَأَكُونَنَّ مِنَ ٱلْقَوْمِ
ٱلضَّآلِّينَ ﴿٧٧﴾

77. Na (usiku wa pili) alipouona mwezi unachomoza alisema (kuwaambia wale marafiki zake wa kikafiri): "Huu (mwezi) ndio Mola wangu." Ulipotua alisema: "Asiponiongoza Mola wangu, bila shaka nitakuwa miongoni mwa watu wapotofu (wapotevu). (Na mola huyu hawezi kuniongoza kwani anakuwa hayupo wakati mwengine)."

فَلَمَّا رَءَا ٱلشَّمْسَ بَازِغَةً قَالَ هَٰذَا رَبِّى هَٰذَآ
أَكْبَرُ ۖ فَلَمَّآ أَفَلَتْ قَالَ يَٰقَوْمِ إِنِّى بَرِىٓءٌ مِّمَّا
تُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾

78. Na (siku ya tatu) alipoliona jua linachomoza alisema (kuwaambia): "Hili (jua) ndilo Mola wangu. Huyu Mola mkubwa kabisa." Lilipotua alisema: "Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha (na Mungu)."

إِنِّى وَجَّهْتُ وَجْهِىَ لِلَّذِى فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ
وَٱلْأَرْضَ حَنِيفًا ۖ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

79. "Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuwa nimewacha dini za upotevu. Mimi (ni Mwislamu) si miongoni mwa washirikina."

وَحَآجَّهُۥ قَوْمُهُۥ ۚ قَالَ أَتُحَٰٓجُّوٓنِّى فِى ٱللَّهِ وَقَدْ
هَدَىٰنِ ۚ وَلَآ أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِۦٓ إِلَّآ أَن
يَشَآءَ رَبِّى شَيْـًٔا ۗ وَسِعَ رَبِّى كُلَّ شَىْءٍ عِلْمًا ۗ أَفَلَا
تَتَذَكَّرُونَ ﴿٨٠﴾

80. Na watu wake wakajadiliana naye (kwa kumwambia Unaacha ibada ya wazee! Utadhurika)! Akasema: "Je, Mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu, na hali yeye ameniongoa? Wala siogopi wale mnaowashirikisha naye. Isipokuwa Mola wangu akipenda jambo (kuwa, basi litakuwa). Mola wangu anakijua vyema kila kitu. Basi je, hamshiki mauidha (Hamzindukani)?"

وَكَيْفَ أَخَافُ مَآ أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ
أَشْرَكْتُم بِٱللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِۦ عَلَيْكُمْ سُلْطَٰنًا ۚ

81. "Na nitawaogopaje hao mnaowashirikisha, hali nyinyi hamwogopi kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kile ambacho hakukiteremshia dalili kwenu (yo yote ya kuonyesha kuwa ni waungu)?

---

hapa kuwa alikuwa kafiri. Na Aya nyingine zimeonyesha kuwa alidumu na ukafiri wake akafa na ukafiri wake. Basi Ulamaa wengine wanasema kuwa huyu ni ami yake tu—si baba yake — japokuwa mara zote Mwenyezi Mungu amemtaja kwa jina la 'Baba yake Ibrahimu, na akakatazwa kumwombea. Na katika *Surat Ibrahimu* — alipokuwa mzee kabisa — alimwombea baba yake na mama yake. Basi huyo ndiye baba yake khasa, si huyu Azar.

Yametajwa haya katika sahifa 306 juzuu ya 3 ya RUUHUL BAYAN na sahifa 319 ya juzuu ya 6 ya MAJMAIL BAYAN na kwenye vitabu vyengine.

76. Hapa Nabii Ibrahimu anawavuta watu kiakili kuacha kuabudu ibada batili—za kuabudu nyota, mwezi na jua na yaliyo kama haya—waabudu ibada ya haki ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

80-81. Kutajwa uweza wa Mwenyezi Mungu na udhaifu wa hao wanaowaabudu.

فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ ۚ إِن كُنتُمْ
تَعْلَمُونَ ﴿٨١﴾

Basi kundi gani katika mawili haya (langu au lenu) linastahiki zaidi kupata amani? Kama nyinyi mnajua jambo (jibuni hili)."

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُم بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ
لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾

82. "(Hapana shaka kuwa) wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na ushirikina kuwa hao ndio watakaopata amani, nao ndio walioongoka."

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ ۚ نَرْفَعُ
دَرَجَاتٍ مَّن نَّشَاءُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٣﴾

83. Na hizi ndizo (baadhi ya) hoja zetu tulizompa Ibrahimu juu ya watu wake. Tunamyanyua katika vyeo yule tumtakaye (kwa kuwa anakwenda mwendo tunaoutaka). Hakika Mola wako ndiye Mwenye hikima (na) ndiye ajuaye.

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۚ كُلًّا هَدَيْنَا ۚ وَنُوحًا
هَدَيْنَا مِن قَبْلُ ۖ وَمِن ذُرِّيَّتِهِ دَاوُودَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ
وَيُوسُفَ وَمُوسَىٰ وَهَارُونَ ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي
الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٤﴾

84. Na tukampa (Ibrahimu mtoto anayeitwa) Ishaqa na (mjukuu anayeitwa) Yaaqubu, wote tukawaongoa. Na Nuhu tulimwongoa zamani (kabla ya kuja Nabii Ibrahimu ulimwenguni). Na katika kizazi chake (Nuhu, tulimwongoa) Daudi na Suleimani na Ayyubu na Yusufu na Musa na Haruni. Na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao mema

وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۖ كُلٌّ مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨٥﴾

85. Na (tukamwongoa) Zakaria na Yahya na Isa na Ilyasi Wote (walikuwa) miongoni mwa watu wema

وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا ۚ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى
الْعَالَمِينَ ﴿٨٦﴾

86. Na (tukamwongoa) Ismaili na Al Yasaa (Ilisha) na Yunusi na Luti. Na wote tukawafadhilisha juu ya walimwengu (wote katika zama zao)

وَمِنْ آبَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ ۖ وَاجْتَبَيْنَاهُمْ
وَهَدَيْنَاهُمْ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٨٧﴾

87. Na (tukawaongoa) baadhi ya baba zao na (baadhi ya) vizazi vyao na (baadhi ya) ndugu zao. Na tukawachagua na kuwaongoza katika njia iliyonyoka.

ذَٰلِكَ هُدَى اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۚ
وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾

88. Huo ni uwongozi wa Mwenyezi Mungu. Kwa huo humwongoza amtakaye katika watu wake (kwa kuwa hawamshirikishi). Na kama wangemshirikisha bila shaka yangaliwaharibikia yale waliyokuwa wakiyatenda.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ۚ فَإِن
يَكْفُرْ بِهَا هَٰؤُلَاءِ فَقَدْ وَكَّلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا بِهَا
بِكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾

89. Hao ndio tuliowapa Vitabu na hukumu (ilimu) na Utume. Kama hawa (makafiri) wakiyakataa hayo, basi tumekwisha yawekea watu wasioyakataa.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۖ فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ ۗ قُل
لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرَىٰ لِلْعَالَمِينَ ﴿٩٠﴾

90. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoa. Basi fuata uwongozi wao. Sema: "Sikuombeni ujira juu ya haya (ninayokufundisheni. Natumika utumwa wa Mwenyezi Mungu). Hayakuwa haya ila ni mauidha kwa watu wote.

---

84. Hapa wanatajwa baadhi ya Mitume wakubwa na watu wao. walioongoka.
88. Kuonyesha kuwa ushirikina unabatilisha wema wote mara moja.
90. Hapa anaambiwa Mtume afuate mwendo wa Mitume hiyo. Na juu ya hivi watungaji mashairi kama Al-

91. Na (Mayahudi) hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama inavyotakiwa kumhishimu, waliposema: "Mwenyezi Mungu hakuteremsha cho chote juu ya binadamu yo yote." (Walisema maneno haya wakati Mtume alipowaambia kuwa Qurani ni kitabu alichoniteremshia Mwenyezi Mungu) Sema: "Ni nani aliyekiteremsha Kitabu alichokileta Musa? Chenye nuru na uwongofu kwa watu, mlichokifanya juzuu juzuu, (zenye vile mnavyotaka vidhihiri) mkadhihirisha. Na yaliyo mengi mkayaficha. Na mmefundishwa (sasa katika hii Qurani) msiyoyajua nyinyi wala baba zenu." Sema: "Mwenyezi Mungu (ndiye aliyeiteremsha hii Qurani na hivyo vyengine)." Kisha waache wacheze katika porojo lao.

وَمَا قَدَرُوا اللّٰهَ حَقَّ قَدْرِهٖٓ اِذْ قَالُوْا مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ عَلٰى
بَشَرٍ مِّنْ شَيْءٍ ۗ قُلْ مَنْ اَنْزَلَ الْكِتٰبَ الَّذِيْ جَآءَ بِهٖ
مُوْسٰى نُوْرًا وَّهُدًى لِّلنَّاسِ تَجْعَلُوْنَهٗ قَرَاطِيْسَ
تُبْدُوْنَهَا وَتُخْفُوْنَ كَثِيْرًا ۚ وَعُلِّمْتُمْ مَّا لَمْ تَعْلَمُوْٓا
اَنْتُمْ وَلَآ اٰبَآؤُكُمْ ۗ قُلِ اللّٰهُ ۙ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِيْ خَوْضِهِمْ
يَلْعَبُوْنَ ﴿٩١﴾

92. Na hii (Qurani) ni Kitabu tulichokiteremsha, chenye baraka nyingi, kinahakikisha yale yaliyokitangulia. Na ili uwaonye (watu wa) Mama wa miji (Makka) na watu walio pembezoni mwake, (ndio maana tukakiteremsha). Na wale wanaoiamini Akhera hukisadiki. Nao huziangalia vizuri Sala zao.

وَهٰذَا كِتٰبٌ اَنْزَلْنٰهُ مُبٰرَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِيْ بَيْنَ يَدَيْهِ
وَلِتُنْذِرَ اُمَّ الْقُرٰى وَمَنْ حَوْلَهَا ۗ وَالَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ
بِالْاٰخِرَةِ يُؤْمِنُوْنَ بِهٖ وَهُمْ عَلٰى صَلَاتِهِمْ
يُحَافِظُوْنَ ﴿٩٢﴾

93. Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Mwenyezi Mungu au mwenye kusema: "Nimeletewa wahyi," na hali hakufunuliwa cho chote; na yule asemaye: "Nitateremsha (ufunuo) kama ule aliouteremsha Mwenyezi Mungu." Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyoshea mikono yao (na kuwaambia): "Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu pasipo haki, na kwa vile mlivyokuwa mkizifanyia kiburi Aya zake;" (ungeona namna gani wanavyopapatika).

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ قَالَ اُوْحِيَ
اِلَيَّ وَلَمْ يُوْحَ اِلَيْهِ شَيْءٌ وَّمَنْ قَالَ سَاُنْزِلُ مِثْلَ مَآ
اَنْزَلَ اللّٰهُ ۗ وَلَوْ تَرٰٓى اِذِ الظّٰلِمُوْنَ فِيْ غَمَرٰتِ الْمَوْتِ
وَالْمَلٰٓئِكَةُ بَاسِطُوْٓا اَيْدِيْهِمْ ۚ اَخْرِجُوْٓا اَنْفُسَكُمْ ۗ
اَلْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُوْنِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُوْلُوْنَ عَلَى
اللّٰهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ اٰيٰتِهٖ تَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٩٣﴾

94. Na (siku ya Kiama tutakwambieni): "Bila shaka nyinyi mmetujia mmoja mmoja (tu, kila mtu

وَلَقَدْ جِئْتُمُوْنَا فُرَادٰى كَمَا خَلَقْنٰكُمْ اَوَّلَ مَرَّةٍ

---

Busyry, Al-Barzanji, Al-Nabhany na wengineo wanavunja daraja zao, bila ya kutanabahi, kama tulivyobainisha katika Juzuu ya tatu katika Aya ya 253.

Katika aliyoyaharibu Sheikh Al Busyry bila kutanabahi ni: (1) "Wakulluhum min Rasuulillahi multamisun . . " yaani "Na Mitume wote wanahitajia kwa Nabii Muhammad awape ukofi mmoja katika ilimu yake iliyo kama bahari au awape kirambisha kinywa tu katika ilimu yake hiyo iliyo kama maji ya mvua . . . . .

(11) "Wawaaqifuuna Ladayhi in-da haddihimuu . . ." yaani "Wamesimama mbele yake Nabii Muhammad kwenye mpaka wao, hawaupindukii, nao ni kama nukta ya ilimu kwa mkabala wa ilimu ya Mtume Muhammad au Irabu moja tu kwa mnasaba wa akili ya Mtume Muhammad." Na yako mengi.

Na katika aliyoyaharibu Sayyid Barzanjy katika maulidi yake ya Nun bila ya kutanabahi kuwa anavunja hishima za Mitume wengine ni kusema:-

(1) "Liummatihim Jaauu yanuubuuna an-hu . . ." yaani "Mitume hao wameziendea umma zao hali ya kuwa wao ni Manaibu tu wa Mtume . . ." (Mwenyewe Mtume wao khaswa ni Nabii Muhammad). Na mengineyo.

peke yake hana mtoto wa kumsaidia wala watumwa wala. . .), kama tulivyokuumbeni mara ya kwanza, na mmeyaacha nyuma yenu tuliyokupeni, na hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi ambao mlidai kuwa ni washirika (wa Mwenyezi Mungu) kwenu. Yamekatika (Makhusiano yaliyokuwa) baina yenu, na yamekupoteeni mliyokuwa mkidai."

وَتَرَكْتُم مَّا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ ۖ وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ
شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَاءُ ۚ لَقَد
ع تَّقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنكُم مَّا كُنتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٩٤﴾

95. Mwenyezi Mungu ndiye mpasuaji (mwoteshaji) wa mbegu na kokwa (zikawa miti). Hutoa mzima katika maiti, naye (pia) ndiye mtoaji maiti katika mzima. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu. Basi mnageuzwa wapi?

إِنَّ اللَّهَ فَالِقُ الْحَبِّ وَالنَّوَىٰ ۖ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ
وَمُخْرِجُ الْمَيِّتِ مِنَ الْحَيِّ ۚ ذَٰلِكُمُ اللَّهُ ۖ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ ﴿٩٥﴾

96. Ndiye anayepambazua mwangaza asubuhi; na ameufanya usiku kuwa mapumziko, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Huo ndio mpimo (mtengenezo) wa Mwenye nguvu(na)ajuaye.

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ
وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٩٦﴾

97. Na Yeye ndiye aliyekuumbieni nyota ili mwongoke kwazo katika viza vya bara na bahari. Hakika tumeeleza vizuri (kila) Aya kwa (nafuu ya) watu wanaojua.

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي ظُلُمَاتِ
الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۗ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٩٧﴾

98. Na Yeye ndiye aliyekuumbeni katika nafsi moja. Na pako (kwa ajili yenu) mahali pa kukaa milele. (Napo ni Akhera), na mahali pa kuwekwa muda mdogo tu (Napo ni duniani). Hakika tumezieleza Aya (hizi) kwa (nafuu ya) watu wanaofahamu.

وَهُوَ الَّذِي أَنشَأَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ فَمُسْتَقَرٌّ
وَمُسْتَوْدَعٌ ۗ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَفْقَهُونَ ﴿٩٨﴾

99. Na yeye ndiye aliyeteremsha maji kutoka mawinguni; na kwayo tunaotesha mimea ya kila kitu. Kisha tunapelekea kuchipua majani ya kijani katika (mimea) hiyo; tukatoa ndani yake punje zilizopangana. Na katika mitende (vinatoka) katika makole yake vishada vyenye kuinama (vinakaribia kufika chini kwa vilivyotia, hata vimekuwa vizito). Na anakuotesheni bustani za zabibu na zaituni na makomamanga, yanayofanana na yasiyofanana. Angalieni matunda yake yanapotoa na (angalieni) kuwiva kwake. Bila shaka katika hayo ziko hoja (kubwa) kwa watu wanaoamini.

وَهُوَ الَّذِي أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ
كُلِّ شَيْءٍ فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا نُّخْرِجُ مِنْهُ
حَبًّا مُّتَرَاكِبًا وَمِنَ النَّخْلِ مِن طَلْعِهَا قِنْوَانٌ دَانِيَةٌ
وَجَنَّاتٍ مِّنْ أَعْنَابٍ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَّانَ مُشْتَبِهًا
وَغَيْرَ مُتَشَابِهٍ ۗ انظُرُوا إِلَىٰ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَيَنْعِهِ ۚ
إِنَّ فِي ذَٰلِكُمْ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٩٩﴾

100. Na (juu ya hivi) wamemfanyia Mwenyezi Mungu majini kuwa washirika wake, hali Yeye ndiye aliyewaumba (si majini). Na wanamsingizia (Mwenyezi Mungu) kuwa ana watoto wa kiume na wa kike. (Wakasema haya) pasipo kujua. Ameepukana (Mwenyezi Mungu) na upungufu, na Yu juu kuliko yale wanayomsifu nayo.

وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ الْجِنَّ وَخَلَقَهُمْ ۖ وَخَرَقُوا لَهُ
ع بَنِينَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٠٠﴾

101. Yeye ndiye Mwumba wa mbingu na ardhi. Inamkinikaje awe na mwana, hali hana mke. Naye ndiye aliyeumba kila kitu (sio baadhi yake kavizaa).

بَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ وَلَدٌ وَلَمْ تَكُن
لَّهُ صَاحِبَةٌ ۖ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ

Naye ni Mjuzi wa kila kitu.

شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٠١﴾

102. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Hakuna anayeabudiwa kwa haki ila Yeye, Mwumba wa kila kitu. Kwa hivyo Mwabuduni yeye (tu). Naye ni Mlinzi wa kila kitu.

ذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ
فَاعْبُدُوهُ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٠٢﴾

103. Macho hayamfikii (kumwona), bali Yeye anayafikia macho (kuyaona na kuwaona hao wenye macho). Naye ni mwenye kujua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri.

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ ۖ وَهُوَ اللَّطِيفُ
الْخَبِيرُ ﴿١٠٣﴾

104. Hakika zimekufikieni hoja kubwa kabisa kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mola wenu (kukuonyesheni kuwa hakuna Mola ila Yeye). Basi anayefunua macho (akaona) ni kwa faida yake mwenyewe; na anayepofoka basi ni khasara yake mwenyewe. Nami si mlinzi wenu (Mimi mwonyaji tu).

قَدْ جَاءَكُمْ بَصَائِرُ مِنْ رَبِّكُمْ ۖ فَمَنْ أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ ۖ
وَمَنْ عَمِيَ فَعَلَيْهَا ۚ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿١٠٤﴾

105. Na namna hivi tunazikariri Aya (wapate kufahamu. Lakini itokeavyo ni) kwamba wanasema: "Umesoma (haya, hakukuletea Mungu)." (Na tumezikariri hivi) ili tuyabainishe kwa watu wanaotaka kujua.

وَكَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ وَلِيَقُولُوا دَرَسْتَ وَلِنُبَيِّنَهُ
لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١٠٥﴾

106. Fuata uliyofunuliwa kutoka kwa Mola wako. Hakuna anayeabudiwa kwa haki ila Yeye. Na ujitenge na washirikina.

اتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ
وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٦﴾

107. Na kama Mwenyezi Mungu angependa (angewatenza nguvu hata) wasingalishirikisha. Na sisi hatukukufanya uwe mlinzi juu yao. Wala wewe si wakili juu yao.

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكُوا ۗ وَمَا جَعَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ
حَفِيظًا ۖ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ﴿١٠٧﴾

108. Wala msiwatukane wale ambao wanawaabudu, kinyume cha Mwenyezi Mungu, wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri zao bila kujua. Namna hivyo tumewapambia kila watu vitendo vyao. Kisha marejeo yatakuwa kwa Mola wao. Naye atawaambia (yote) waliyokuwa wakiyatenda.

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ
عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ كَذَٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمْ
ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ مَرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٠٨﴾

109. Na (makafiri) waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa viapo vyenye nguvu, kama ikiwafikia miujiza (waitakayo) wataiamini. Sema: "Miujiza iko kwa Mwenyezi Mungu (haiko katika mikono yangu). Na (nyinyi Waislamu mnaotaka iteremke miujiza hiyo tunakuambieni). "Ni kitu gani kilichokutambulisheni ya kuwa itakapofika (miujiza hiyo) hawataamini?"

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِنْ جَاءَتْهُمْ آيَةٌ
لَيُؤْمِنُنَّ بِهَا ۚ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ ۖ وَمَا
يُشْعِرُكُمْ أَنَّهَا إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٩﴾

---

Na katika aliyoyaharibu Sheikh An Nabhany ni kusema:- (1) Ya Nabiyyan Minjun-dihil Anbiyaau. "yaani" "Ee Mtume ambaye Mitume ni katika askari zake. . . ."

(11) "Hum Jamiy-an adhwaauhuu. . . ." yaani "Mitume yote hiyo ni miangaza tu, nuru yake imepata kwa Nabii Muhammad" Na kama haya mengi kabisa.

91. Katika pupa la Mayahudi kutaka kumkataa Mtume walisema: "Mwenyezi Mungu hakupata kumteremshia kiumbe cho chote." Basi Mwenyezi Mungu Anawatahayarisha na Kuwasimanga.

110. (Hawataamini); na tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama wasivyoamini mara ya kwanza; na tutawaacha katika maasiya yao wakitangatanga ovyo.

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِ أَوَّلَ
مَرَّةٍ وَنَذَرُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

111. Na lau kama tungewateremshia Malaika (kuwashuhudilia Ujumbe wa Nabii Muhammad kama walivyotaka), na wafu wakazungumza nao (kuwa haya ni kweli), na tukawakusanyia kila kitu mbele yao (kikawambia haya pia), wasingaliamini isipokuwa atake Mwenyezi Mungu (kuwatenza nguvu mpaka waamini). Lakini wengi wao wamo ujingani.

وَلَوْ أَنَّنَا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ
وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا
إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُونَ ﴿١١١﴾

112. Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui; (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani katika) majini. Baadhi yao wanawafunulia wenziwao maneno ya kupambapamba ili kuwadanganya. Na kama Mola wako angalipenda wasingalifanya hayo, (angewalazimisha kwa nguvu kutii). Basi waache na uwongo wao.

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيَاطِينَ الْإِنْسِ
وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ
غُرُورًا وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

---

93. Yanatajwa yatakayowapata wabaya tangu saa ya kutoka roho mpaka saa ya kuhisabiwa.

94. Yanatajwa yatakayowakuta wabaya siku ya Kiama; kuwa (a) hawatakuwa na Mwombezi na (b) hata wakitoa kikomboleo gani, hakitakubaliwa.

Sharia husema
Shida na mashaka
Shufaa ya Tumwal
Huwa mbali naye

Aso thawabu
Yatamsibu
Mahabubu
Na kumwegema.

95-103. Baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu na neema zake juu ya viumbe vyake.

108. Hapa wanakatazwa Waislamu kutukana dini za watu wengine. Ukitaka kumbainishia mtu haki mbainishie kwa maneno mazuri, matamu, ya upole. Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni.

109. Hapa wanakatishwa tamaa Waislamu juu ya makafiri hao washindani kuwa hawataamini hata wakiteremshiwa miujiza hiyo wanayoitaka.

111. Hapa inatajwa kuwa hata lau hao makafiri wakaidi wangeonyeshwa hiyo miujiza wanayoitaka, nao wasingeamini. Kama huko kutaka kwao (a) Wateremke Malaika wawape khabari kuwa kweli Nabii Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu; (b) Wafufuliwe waliokufa wawape habari hii pia; (c) Bali na kila kitu kije mbele yao kuwapa khabari hii.

112. Katika maelezo ya Aya hii waliyoifanya ni ya 113 wametia ukafiri wao mwengine wa kukataa viumbe vinavyoitwa majini. Kila Mwislamu anajua kuwa kuna Malaika na Binaadamu na Majini na wengineo. Na kila mmoja katika hao ameumbwa kwa vitu (zana) asivyoumbiwa mwenziwe. Malaika wameumbwa kwa Nuru. Binaadamu, Qurani yote nzima inasema, wameumbwa kwa Maji na kwa Udongo; na Majini wameumbwa kwa Moto. Qurani yote nzima imejaa katika kutaja kuumnbwa kwa Binaadamu kuwa wameumbwa (a) *Min Tyn* (b) *Min Sulaalatin Min Tyn* (c) *Min Turaabin* (d) *Min Salsaalin* (e) *Hamain* (f) *Min Main* (g) *Min Main Mahyn*. Na imejaa katika kutaja kuumbwa Majini na Mashetani (a) *Min Naar* (b) *Min Naaris Samuum*.

Wao wanajifanya wanajua hakika kuliko Mungu, wanamsuta Mwenyezi Mungu wanaandika hivi: "Maneno haya: *Watu na Majini*, ambayo yanapatikana katika Aya nyingi za Qurani hayaonyeshi viumbe vya namna mbili